

القرآن الحكيم

QURANI TAKATIFU

Swahili Quran Translation

by
Sheikh Abdullah Saleh Al-Farsy
(Former Chief Kadhi of
Zanzibar & Kenya)

31. Akasema, "Basi makusudio yenu (mengine) ni nini, Enyi mliotumwa?"

32. Wakasema: "Hakika sisi tumetumwa Tukawaangamize wale watu waovu (watu wa Nabii Luti)."

33. "Ili tuwatupie juu yao mawe ya udongo (wa Motoni)".

34. "Yaliyotiwa alama kwa Mola wako kwa ajili ya hao watu wanaopindukia mipaka katika maasia."

35. (Mwenyezi Mungu anasema): "Kwa hivyo Tukawatoa wale walioamini waliokuwa humo (ili adhabu isiwaifike)".

36. Lakini Hatukupata humo ila nyumba moja tu yenye Waislamu.

37. Na (baada ya kuwaangamiza) Tukaacha humo alama kwa ajili ya wale wanaoogopa adhabu iumizayo.

38. Na katika (habari za) Musa (ziko alama vile vile), Tulipompeleka kwa Firauni na hoja wazi kabisa.

39. Lakini akakengeuka (asiyafuate hayo) kwa sababu ya nguvu zake na akasema: "Huyu ni mchawi au ni mwandawazimu".

40. Basi Tukamkamata (tukamtia mkononi) yeye na majeshi yake na Tukawatupa baharini, na mwenyewe alikuwa mlaumiwa.

41. Na katika (habari za), Adi (ziko alama kadhalika). (Kumbusha) Tulipowapelekea upepo wa papazi uangamizao.

42. Haukuacha chochote ulichokijia ila ulikifanya kama kamba mbovu.

43. Na katika (habari za) Thamudi (ziko alama vile vile), (Kumbusha) walipoambiwa: "Jifurahisheni kwa muda mdogo tu. (Sasa hivi itakuja adhabu ikuangamizeni)."

44. Wakaasi (wakakataa kwa jeuri) amri ya Mola wao; mara moto wa Radi uliwatoa roho zao na huku wanaona.

قَالَ فَمَا خَطْبُكُمْ أَيُّهَا الْمُرْسَلُونَ ۝

قَالُوا إِنَّا أُرْسِلْنَا إِلَىٰ قَوْمٍ مُّجْرِمِينَ ۝

يُرْسِلَ عَلَيْهِمْ حِجَارَةً مِّنْ طِينٍ ۝

مُسَوَّمَةً عِندَ رَبِّكَ لِلْمُسْرِفِينَ ۝

فَأَخْرَجْنَا مَن كَانَ فِيهَا مِّنَ الْمُؤْمِنِينَ ۝

فَمَا وَجَدْنَا فِيهَا غَيْرَ بَيْتٍ مِّنَ الْمُسْلِمِينَ ۝

وَتَرَكْنَا فِيهَا آيَةً لِلَّذِينَ يَخَافُونَ الْعَذَابَ الْأَلِيمَ ۝

وَفِي مِثْلِهِ إِذْ أَرْسَلْنَاهُ إِلَىٰ فِرْعَوْنَ بِسُلْطَانٍ مُّبِينٍ ۝

فَتَوَلَّىٰ بِرْكَيْهِ وَقَالَ سِجْرًا مَّجْنُونٌ ۝

فَأَخَذْنَاهُ وَجُودَهُ فَنَبَذْنَاهُ فِي الْيَمِّ وَهُوَ مُلَيَّمٌ ۝

وَفِي عَادٍ إِذْ أَرْسَلْنَا عَلَيْهِمُ الرِّيحَ الْعَقِيمَ ۝

مَا تَذَرُ مِن شَيْءٍ أَنتَ عَلَيْهِ إِلَّا جَعَلَتْهُ كَالْهَبِ ۝

وَفِي ثَمُودَ إِذْ قِيلَ لَهُم تَسْعُوا حَتَّىٰ حَبِينٍ ۝

فَعَتَوْا عَنْ أَمْرِ رَبِّهِمْ فَأَخَذْنَا مِنْهُمُ الصُّعْقَةَ وَهُمْ يَنْظُرُونَ ۝

31-37. Kunatajwa kuangamizwa kwa watu wa Nabii Luti.

38-46. Kunatajwa kuangamiya uma za Mitume wengine.

45. Basi hawakuweza kusimama (kukimbia) wala hawakuweza kujipigania

46. Na (wakumbushe) watu wa Nuhu (tuliowaangamiza) pia, (waliokuwa) kabla (ya hawa). Hakika wao walikuwa watu maasi.

47. Na mbingu Tumezifanya kwa kudra (yetu); na hakika Sisi ndio wenye uweza (wa kila kitu).

48. Na ardhi Tumeitandaza; basi Watandazaji Wazuri walioje Sisi!

49. Na katika kila kitu Tumeumba dume na jike ili mpate kufahamu.

50. Basi kimbilieni kwa Mwenyezi Mungu, mimi kwenu ni Muonyaji waziwazi ninayetoka Kwake.

51. Wala msimfanye mwingine kuwa aabudiwaye pamoja na Mwenyezi Mungu. Bila shaka mimi ni Muonyaji niliye dhahiri kwenu ninayetoka Kwake.

52. Basi ndiyo vivi hivi; hakuna Mtume yoyote aliyewajia wale wa kabla yao (hawa Makureshi) ila walisema: "Huyu ni mchawi au mwendawazimu."

53. Je! Wameusia kwa (jambo) hili? (La; hawakuusia chochote); lakini (wote) wao ni watu waovu.

54. Basi waachilie mbali, nawe hutalaumiwa (ukiwaachilia mbali hivyo).

55. Na endelea kuwakumbusha; maana ukumbusho huwafaa wanaoamini.

56. Sikuwaumba majini na watu ila wapate kuniabudu.

57. Sitaki kwao riziki wala Sitaki wanilishe.

58. Kwa yakini Mwenyezi Mungu ndiye Mtoaji wa riziki, Mwenye nguvu, Madhubuti.

59. Hakika wale waliodhulumu (katika uma huu) watakuwa na sehemu (yao ya adhabu) kama sehemu ya wenzao (waliotangulia), basi wasinihimize.

60. Adhabu kali itawathubutikia wale walioikanusha siku yao wanayoahidiwa.

فَمَا اسْتَطَاعُوا مِنْ قِيَامٍ وَمَا كَانُوا مُتَسَارِعِينَ ۝

وَقَوْمٌ نُوْجِدُ مِنْ قَبْلِ اِنَّهُمْ كَانُوا قَوْمًا فَاسِقِينَ ۝

وَالسَّمَاءَ بَنَيْنَاهَا بِاَيْدٍ وَإِنَّا لَمُوسِعُونَ ۝

وَالْأَرْضَ فَرَشْنَاهَا فَنِعْمَ الْمُهْدُونَ ۝

وَمِنْ كُلِّ شَيْءٍ خَلَقْنَا زَوْجَيْنِ لَعَلَّكُمْ

تَذَكَّرُونَ ۝

فَقَرِّءُوا آيَةَ اللَّهِ الَّتِي كُتِبَتْ لَهُمْ نَذِيرٌ مُبِينٌ ۝

وَلَا تَجْعَلُوا مَعَ اللَّهِ إِلَهًا آخَرَ إِنِّي لَكُمْ مِنْهُ نَذِيرٌ

مُبِينٌ ۝

كَذَلِكَ مَا آتَى الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ مِنْ رَسُولٍ إِلَّا قَالُوا

سَاحِرٌ أَوْ مَجْنُونٌ ۝

أَتَوَصَّوهُمْ بِبَلٍ هُمْ قَوْمٌ طَاغُونَ ۝

فَقُلْ عَنْهُمْ فَمَا أَنْتَ بِمَلُومٌ ۝

وَذَكِّرْ فَإِنَّ الذِّكْرَ تَنْفَعُ الْمُؤْمِنِينَ ۝

وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّ وَالْإِنْسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ ۝

مَا أُرِيدُ مِنْهُمْ مِنْ رِزْقٍ وَمَا أُرِيدُ أَنْ يُطْعَمُوا ۝

إِنَّ اللَّهَ هُوَ الرَّزَّاقُ ذُو الْقُوَّةِ الْمَتِينُ ۝

فَأَنَّ لِلَّذِينَ ظَلَمُوا ذُنُوبًا مِثْلَ ذُنُوبِ أَصْحَابِهِمْ

فَلَا يَسْتَعْجِلُونَ ۝


فَوَيْلٌ لِلَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ يَوْمِهِمُ الَّذِي

يُوعَدُونَ ۝

49. Hii ni katika zile Aya zilizosema maneno ambayo ndiyo kwanza sasa yamefahamika. Na haya ni kama yale yaliyomo katika Aya ya 36 ya Surat Yasin.

52-53. Kuonyesha kuwa kupingwa Nabii Muhammad si kiroja. Mitume wote walipingwa.

56. Hii ni moja katika sababu zilizotajwa kwa ajili ya kuumbwa vilivyoundwa. Na sababu nyingine imetajwa katika Aya ya 12 ya Suratul Talaq. Basi yale maneno yanayosema: "Lawlaaka Lawlaaka Maakhalaqtul Afilaak" si maneno ya kutegemewa.



Ina Aya 49

SURATUT TUR

Ina Makara 2

(Imeteremka Makka)

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa, na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

1. Naapa kwa Mlima (huo aliosemezewa Musa)

وَالطُّورِ ۝

2. Na kwa Kitabu kilichoandikwa (kila anayotaka Mwenyezi Mungu yaandikwe)

وَكِتَابٍ مُّسْطُورٍ ۝

3. (Kilichoandikwa) katika karatasi ya ngozi (iliyosafi na) kikakunjuliwa (kisomwe)

فِي رَقٍّ مَنْشُورٍ ۝

4. Na kwa (hiyo) Nyumba inayozuriwa (daima)

وَالْبَيْتِ الْمَعْمُورِ ۝

5. Na kwa sakafu (mbingu) zilizonyanyuliwa juu

وَالسَّقْفِ الْمَرْفُوعِ ۝

6. Na kwa bahari zilizojazwa (maji)

وَالْبَحْرِ الْمَسْجُورِ ۝

7. Kwa yakini adhabu ya Mola wako itatokea

إِنَّ عَذَابَ رَبِّكَ لَوَاقِعٌ ۝

8. Hakuna atakayeizuia

مَالَهُ مِنْ دَافِعٍ ۝

9. Siku zitakapotikisika mbingu kwa mtikisiko (mkubwa kabisa)

يَوْمَ تَمُورُ السَّمَاءُ مَوْرًا ۝

10. Na majabali (yang'oke), yawe yanakwenda (angani) mwendo (mkubwa).

وَلَيَسِيرُ الْجِبَالُ سَيْرًا ۝

11. Basi adhabu siku hiyo itawapata wakadhibishao

فَوَيْلٌ لِلَّذِينَ كَفَرُوا يَوْمَ يَكُونُ

12. Ambao wanacheza (sasa) katika mambo ya upuuzi.

الَّذِينَ هُمْ فِي خَوْضٍ يَلْعَبُونَ ۝

13. Siku watakaposukumwa katika moto wa Jahanamu msukumo (wa nguvu).

يَوْمَ يُدْعَوْنَ إِلَى نَارِ جَهَنَّمَ دُخَاءً ۝

14. (Na huku wanaambiwa): "Huu ndio ule Moto ambao mlikuwa mkiukadhibisha."

هَذِهِ النَّارُ الَّتِي كُنْتُمْ بِهَا تُكَذِّبُونَ ۝

15. "Basi, Je! Huu ni uchawi (küni macho) au hamuoni (kuwa mnaungua hivi)?"

أَفَحَسِبْتُمْ أَنْ تُتْرَكُوا أَنْ تَبْصُرُونَ ۝

16. "Uingieni, mkistahamili au msistahamili, ni mamoja kwenu; mnalipwa mliyokuwa mkiyatenda."

أَصْلَوْهَا فَاصْبِرُوا أَوْ لَا تَصْبِرُوا سَوَاءٌ عَلَيْكُمْ ۝

إِنَّمَا تُجْزَوْنَ مَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ۝

17. Kwa yakini wamchao Mwenyezi Mungu watakuwa katika mabustani na neema

إِنَّ الْمُتَّقِينَ فِي جَنَّاتٍ وَعُيُُنٍ ۝

18. Wakifurahia yale Aliyowapa Mola wao; na Mola wao amewalinda na adhabu ya Moto uwakao (kwa nguvu kabisa).

فَكَهْنٍ يَمَّا أَنَّهُمْ رَبُّهُمْ ۖ وَوَقَّعَهُمْ رَبُّهُمْ عَذَابَ الْجَحِيمِ ۝

19. (Wataambiwa watu wema): "Kuleni na kunyweni kwa raha kabisa kwa sababu ya hayo mliyokuwa mkiyatenda"

كُلُوا وَاشْرَبُوا هَنِيئًا بِمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ۝

20. Watakuwa wameegemea juu ya viti vya fahari vilivyopangwa safu safu, na Tutawaoza wanawake wanaopendeza wenye macho ya vikombe (makubwa).

مُشْكِينَ عَلَى سُرُرٍ مَّصْفُوفَةٍ ۖ وَزَوَّجْنَاهُمْ بِحُورٍ عِينٍ ۝

21. Na wale walioamini na wakafuatwa na vizazi vyao na watoto wao katika imani, Tutawakutanisha nao hao jamaa zao, wala Hatutawapunja kitu katika (thawabu za) vitendo vyao; kila mtu atalipwa kwa kile alichokichuma.

وَالَّذِينَ آمَنُوا وَاتَّبَعَتْهُمْ ذُرِّيَّتُهُمْ بِإِيمَانٍ أَلْحَقْنَا بِهِمْ ذُرِّيَّتَهُمْ وَمَا أَلَتْنَاهُمْ مِنْ عَمَلِهِمْ مِنْ شَيْءٍ ۚ كُلُّ امْرِئٍ بِمَا كَسَبَ رَهِينٌ ۝

22. Na Tutawapa (kila namna ya) Matunda na (kila namna za) nyama, kama vile watakavyopenda.

وَأَمَدَدْنَاهُمْ بِفَاكِهَةٍ وَلَحْمٍ مِّمَّا يَشْتَهُونَ ۝

23. Watapeana humo gilasi (zilizojaa vinywaji) visivyoleta maneno ya upuuzi wala ya dhambi.

يَتَنَزَّلُونَ فِيهَا كَأْسًا لَّا لَعْفُ فِيهَا وَلَا تَأْثِيمٌ ۝

24. Iwe wanawapitia watumishi wao (wanaopendeza) kama kwamba ni lulu zilizomo ndani ya chaza (shaza) (ndio kwanza zimepasuliwa).

وَيُطَوَّفُ عَلَيْهِمْ غِلْمَانٌ لَّهُمْ كَأْسٌ لَّهُمْ لَوْلَوْ مَكْنُونٌ ۝

25. Wataelekeana wao kwa wao wanaulizana, (wanazungumza).

وَأَقْبَلَ بَعْضُهُمْ عَلَى بَعْضٍ يَتَسَاءَلُونَ ۝

26. Waseme: "Tulikuwa zamani pamoja na watu wetu tukimuogopa (Mwenyezi Mungu)."

قَالُوا إِنَّا كُنَّا قَبْلُ فِي أَهْلِنَا مُشْفِقِينَ ۝

27. "Basi Mwenyezi Mungu Ametufanyia ihsani, (ametutia Peponi) na Ametuokoa na adhabu ya pepo za Moto."

فَمَنْ أَلَّهِ عَلَيْهِمْ وَأَوْقَعْنَا عَذَابَ الْمُؤْمِرِ ۝

28. "Hakika sisi zamani tulikuwa tukimuabudu Yeye (tu Mwenyezi Mungu): Hakika Yeye ndiye Mwema, Mwenye rehema."

إِنَّا كُنَّا مِنْ قَبْلُ نَدْعُوهُ ۚ إِنَّهُ هُوَ الْبَرُّ الرَّحِيمُ ۝

29. Basi endelea kuwakumbusha. Na wewe kwa neema za Mola wako si mchawi wala si mwendawazimu, (si kama wanavyosema).

فَذَكِّرْ فَمَا أَنْتَ بِنِعْمَتِ رَبِّكَ بِكَاهِنٍ وَلَا مَجْنُونٍ ۝

17-28. Yanatajwa watakayoyapata watu wema, na yapi waliyoyafanya hata wakapata haya.

29-47. Hapa wanasimangwa hao Maqureshi kwa ya uwongo wao na wanatajiwa yatakayowafika mwisho wao.

30. Ndiyo wanasema kuwa: “Huyu (Muhammad) ni mtunga mashairi, tunamtazamia kupatikana na mauti (kama walivyokufa washairi wengine)?”

31. Sema: “Ngojeeni, na mimi pia ni pamoja nanyi katika wangojeao. (Sifi mimi tu peke yangu, na nyinyi mtakufa vile vile).”

32. Au hizo akili zao kubwa (wanazojisifu kwazo) ndizo zinazowaamrisha (kusema maneno) haya (yasiyokuwa na akili), au wao ni watu majeuri tu?

33. Au ndio wanasema (hivi) kuwa hii (Qurani) ameitunga (yeye mwenyewe Muhammad)? Bali wao hawaamini lolote.

34. Basi nawalete Hadithi kama hizi; ikiwa wanasema kweli (kuwa hii Qurani kaitunga Nabii Muhammad).

35. Je! Wameumbwa pasipo kitu, au wao ndio waliojumba.

36. Au wameumba mbingu na ardhi? Bali hawana yakini (ya jambo lolote).

37. Au wanazo khazina za Mola wako au wao ndio wapitishaji amri (zao)?

38. Au wanayo ngazi (wanayopanda wakenda mbinguni) wakasikilizia (yanayosemwa huko)? Basi msikiaji wao alete dalili iliyo wazi (ya ukweli wa jambo hili).

39. Au yeye (Mwenyezi Mungu) Anao watoto wanawake; nanyi mnao watoto wanaume?

40. Au unawaomba ujira, kwa hivyo wanaelemewa na gharama?

41. Au iko kwao (ilimu ya) ghaibu; nao wameandika (hiyo; kwa hivyo hawahitaji ilimu ya Ghaibu unayowatajia)?

42. Au wanataka kufanya vitimbi (tu basi)? Lakini waliokufuru ndio watakaotegwa (watakaonaswa kwa vitimbi vyao hivyo).

43. Au yuko kwao Mola (anayeabudiwa kwa haki) asiyekuwa Mwenyezi Mungu? Mwenyezi Mungu Ametakasika na hao wanaowashirikisha naye.

44. Na hata wangeona kitu kinatoka upande wa mbinguni kinaanguka wangesema: “Ni mawingu

أَمْ يَقُولُونَ شَاعِرٌ تَتَرَبَّصُّ بِهِ رَيْبَ الْمُنُونِ ۝

قُلْ تَرَبَّصُوا فَإِنِّي مَعَكُمْ مِنَ الْمُرَاصِلِينَ ۝

أَمْ تَأْمُرُهُمْ أَحْلَامُهُمْ بِهَذَا أَمْ هُمْ قَوْمٌ طَاغُونَ ۝

أَمْ يَقُولُونَ تَقَوَّلَهُ، بَلْ لَا يُؤْمِنُونَ ۝

فَلْيَأْتُوا بِحَدِيثٍ مِثْلِهِ إِن كَانُوا صَادِقِينَ ۝

أَمْ خُلِقُوا مِنْ غَيْرِ شَيْءٍ أَمْ هُمُ الْخَالِقُونَ ۝

أَمْ خَلَقُوا السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ، بَلْ لَا يُوقِنُونَ ۝

أَمْ عِنْدَهُمْ خَزَائِنُ رَيْكِ أَمْ هُمُ الْمُصْطَرُّونَ ۝

أَمْ لَهُمْ سُلَّمٌ يَسْتَمْعُونَ فِيهِ، فَلْيَأْتِ مُسْتَمْعِيهِمْ بِسُلْطَانٍ مُبِينٍ ۝

أَمْ لَهُ الْبَنَاتُ وَلَكُمُ الْبَنُونَ ۝

أَمْ تَسْأَلُهُمْ أَجْرًا فَهُمْ مِنْ مَغْرَمٍ مُثْقَلُونَ ۝

أَمْ عِنْدَهُمُ الْغَيْبُ فَهُمْ يَكْتُبُونَ ۝

أَمْ يُرِيدُونَ كَيْدًا فَالَّذِينَ كَفَرُوا هُمْ الْمَكِيدُونَ ۝

أَمْ لَهُمْ إِلَهٌ غَيْرُ اللَّهِ سُبْحَانَ اللَّهِ عَمَّا يُشْرِكُونَ ۝

وَإِنْ يَرَوْا كِسْفًا مِنَ السَّمَاءِ سَاقِطًا يَقُولُوا

yaliyobebana (tu, si alama kuwa adhabu inakuja wala nini).”

45. Basi waache mpaka wakutane na siku yao ambayo zitatoka roho zao siku hiyo

46. Siku ambayo hila zao hazitawafaa hata kidogo wala hawatanusuriwa.

47. Na kwa yakini wale waliodhulumu watakuwa na adhabu nyingine (huku duniani kabla ya Akhera). Lakini wengi wao hawajui lolote.

48. Na ingoje hukumu ya Mola wako. Na hakika wewe uko mbele ya macho Yetu. Na Mtukuze kwa kumsifu Mola wako unaposimama (kusali Adhuhuri na Laasiri)

49. Na katika usiku pia Mtukuze (kwa kusali Magharibi na Isha); na zichwapo nyota (kwa kusali Sala ya Alfajiri).

سَحَابٌ مَّرْكُومٌ ۝

فَذَرْهُمْ حَتَّى يُلَاقُوا يَوْمَهُمُ الَّذِي فِيهِ يُصْعَقُونَ ۝

يَوْمَ لَا يُغْنِي عَنْهُمْ كَيْدُهُمْ شَيْئًا وَلَا هُمْ

يُنصَرُونَ ۝

وَأَنَّ لِلَّذِينَ ظَلَمُوا عَذَابًا دُونَ ذَلِكَ وَلَكِنَّ

أَكْثَرَهُمْ لَا يَعْلَمُونَ ۝

وَاصْبِرْ بِحُكْمِ رَبِّكَ فَإِنَّكَ بِأَعْيُنِنَا وَسَبِّحْ بِحَمْدِ

رَبِّكَ حِينَ تَقُومُ ۝

وَمِنَ اللَّيْلِ فَسَبِّحْهُ وَإِدْبَارَ النُّجُومِ ۝



Ina Aya 62

SURATUN NAJM

Ina Makara 3

(Imeteremka Makka)

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuncernesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuncernesha neema ndogo ndogo.

1. Naapa kwa nyota zinapoanguka. (zinapokuchwa)

2. Kwamba mtu wenu (huyu Nabii Muhammad) hakupotea (kwa ujinga) wala hakukosa, (na hali ya kuwa anajua);

3. Wala hasemi kwa matamanio (ya nafsi yake).

4. Hayakuwa haya (anayosema) ila ni Wahyi (ufunuo), uliofunuliwa (kwake)

5. Amemfundisha (Malaika) Mwenye nguvu sana

6. Mwenye uweza. Na yeye (huyu Jibrili) akalingana sawa sawa

7. Na yeye yu katika upeo wa kuona, (Horizon) (katika mbingu kwa) juu kabisa.

8. Kisha akakaribia (kwa Mtume) na akateremka

9. Ukawa (ukaribu wao) ni kama baina ya upinde na upinde au karibu zaidi.

10. Na Akamfunulia huyo Mtumwa wake (Mwenyezi Mungu) Aliyoyafunua.

11. Moyo haukusema uwongo uliyoyaona. (Moyo wake ulisadikisha haya yaliyotokea).

12. Je! Mnabishana naye juu ya yale anayoyaona (daima)?

13. Na (Mtume) akamuona (Jibrili) mara nyingine (kwa sura ile yake ya Kimalaika katika usiku wa Müräji)

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

وَالنَّجْمِ إِذَا هَوَىٰ ۝

مَا ضَلَّ صَاحِبُكُمْ وَمَا غَوَىٰ ۝

وَمَا يَنْطِقُ عَنِ الْهَوَىٰ ۝

إِنْ هُوَ إِلَّا وَحْيٌ يُوحَىٰ ۝

عَلَّمَهُ شَدِيدُ الْقُوَىٰ ۝

ذُو مِرَّةٍ ۖ فَاسْتَوَىٰ ۝

وَهُوَ بِالْأُفُقِ الْأَعْلَىٰ ۝

ثُمَّ دَنَا فَتَدَلَّىٰ ۝

فَكَانَ قَابَ قَوْسَيْنِ أَوْ أَدْنَىٰ ۝

فَأَوْحَىٰ إِلَىٰ عَبْدِهِ مَا أَوْحَىٰ ۝

مَا كَذَبَ الْفُؤَادُ مَا رَأَىٰ ۝

أَفَتُمَارُونَهُ عَلَىٰ مَا يَرَىٰ ۝

وَلَقَدْ رَآهُ نَزْلَةً أُخْرَىٰ ۝

1-18. Inatajwa habari ya Müräji ya Mtume — kwenda mbinguni.

14. Penye Mkunazi wa kumalizikia (Mambo yote).

عِنْدَ سِدْرَةِ الْمُنْتَهَى ⑭

15. Karibu yake ndiyo kuna hiyo Bustani, (Pepo) itayokaliwa (maisha na hao watu wema).

عِنْدَهَا جَنَّةُ الْمَأْوَى ⑮

16. Kilipoufunika Mkunazi huo kilichoufunika (katika mambo ya kiajabu ya kimbinguni)

إِذْ يَغْشَى السِّدْرَةَ مَا يَغْشَى ⑯

17. Jicho halikuhangaika wala halikuruka mpaka (uliwekewa).

مَا زَاغَ الْبَصَرُ وَمَا طَغَى ⑰

18. Kwa yakini aliona (Nabii Muhammad) mambo makubwa kabisa katika alama, (Qudra) za Mola wake.

لَقَدْ رَأَى مِنْ آيَاتِ رَبِّهِ الْكُبْرَى ⑱

19. Je! Mumewaona Lata na Uzza

أَفَرَأَيْتُمُ اللَّاتَ وَالْعُزَّىٰ ⑲

20. Na Manata, (mungu wenu) mwingine wa tatu, (kuwa ndio waungu hao badala ya Mwenyezi Mungu)?

وَمَنْوَةُ الثَّالِثَةِ الْاُخْرَى ⑳

21. Je! Nyinyi muna watoto wa kiume na Yeye ana watoto wa kike?

أَلَكُمْ الذَّكَرُ وَلَهُ الْأُنثَى ㉑

22. Huo ni mgawanyo wa dhuluma! Basi (mnamdhulumu Mungu!)

تِلْكَ إِذَا قِسْمَةٌ ضِيزَى ㉒

23. Hayakuwa haya (majina ya Lata, mungu mwanamke, na Al-uzza, mungu mwanamke mwenye enzi, na Manata, mungu mwanamke anayeneemesha) ila ni majina tu mliyowapa nyinyi na baba zenu (masanamu hayo; wala hawana lao jambo). Mwenyezi Mungu Hakuteremsha dalili juu ya hayo. Hawafuati ila dhana na zinayoyapenda nafsi (zao). Na kwa yakini uwongofu umewajia kutoka kwa Mola wao (lakini hawataki tu kuufuata).

إِنْ هِيَ إِلَّا أَسْمَاءٌ سَمَّيْتُمُوهَا أَنْتُمْ وَ آبَاؤُكُمْ
مَا أَنْزَلَ اللَّهُ بِهَا مِنْ سُلْطَانٍ إِنْ يَتَّبِعُونَ
إِلَّا الظَّنَّ وَمَا تَهْوَى الْأَنْفُسُ وَلَقَدْ جَاءَهُمْ مِنْ
رَبِّهِمْ الْهُدَى ㉓

24. Je! Mwanaadamu anaweza kupata kila anachotamani?

أَمْرِ لِلْإِنْسَانِ مَا تَمَنَّى ㉔

25. Ni ya Mwenyezi Mungu tu Akhera na dunia.

يَا قُلِ لِلَّهِ الْآخِرَةُ وَالْأُولَى ㉕

26. Na wako Malaika wangapi mbinguni, ambao uombezi wao hautafaa chochote isipokuwa

وَكَمٍ مِّنْ مَّلَكٍ فِي السَّمَوَاتِ لَا تُغْنِي شَفَاعَتُهُمْ شَيْئًا

19-23. Wanatolewa maanani kwa kuabudu masanamu na kwa kuwafanya waungu wao hao katika umbo la kike; na wao wenyewe wanawazarau, (wanawadharau) wanawake na kuwazika wazima pia.

21. Wao hawapendi watoto wanawake. Na juu ya hayo wanamnasibishia Mungu kuwa ana watoto wanawake.

24-26. Kuonyeshwa viumbe kuwa mambo yote yamo katika mikono ya Mwenyezi Mungu Akiyafuata anayoyataka Mwenyezi Mungu ndipo atakapopata salama siku ya Kiama.

baada ya Mwenyezi Mungu kutoa idhini kwa Amtakaye na kumridhia.

27. Hakika wale wasioamini Akhera wanawaita Malaika kwa majina ya kike.

28. Nao hawana ujuzi wowote kwa hayo (wanayoyasema), hawafuati ila dhana tu: na kwa hakika dhana haisaidii chochote mbele ya haki.

29. Basi jiepuche na wale waupao kisogo ukumbusho Wetu huu, (Qurani) Na wala hawataki ila maisha (Starehe) ya dunia.

30. Huu ndio mwisho wao katika kujua (kwao). Hakika Mola wako ndiye Amjuaye anayepotea njia Yake, na Ndiye Amjuaye anayeongoka.

31. Ni vya Mwenyezi Mungu (tu vyote) vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini. (Ameleta amri hizi na makatazo haya) ili Awalipe wabaya kwa hayo wanayoyatenda, na kuwalipa mema wale wanaofanya mema.

32. Ambao wanajiepusha na madhambi makuu na vitendo vichafu; isipokuwa makosa hafifu, (hakuna aliyesalimika nayo); bila shaka Mola wako ndiye Mwenye maghufira mengi. Yeye ndiye Anayekujueni sana tangu Alipokuumbeni katika ardhi, na mlipokuwa mimba matumboni mwa mama zenu. Basi msizitakase (msizisifu) nafsi zenu; Yeye Anamjua sana aliyetakasika (na asiyetakasika).

33. Je! Umemuona yule aliyegeuka?

34. Na akatoa kidogo (utiifu wake) kisha akajizuia.

35. Je! anayo ilimu ya yasiyoonekana, (Ilimu Ghaib), akaona, (kuwa haya aliyokuja nayo Nabii Muhammad siyo haki)?

36. Au hakuambiwa yaliyomo katika vitabu vya Musa?

37. Na vya Ibrahimu aliyetimiza ahadi (ya Mwenyezi Mungu)

إِلَّا مَنْ بَعْدَ أَنْ يَأْذَنَ اللَّهُ لِمَنْ يَشَاءُ وَيَرْضَىٰ ۚ
إِنَّ الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِالْآخِرَةِ لَيَسْئُونَ الْمَلَائِكَةَ
تَسْيِئَةً ۚ الْأَنْثَىٰ ۝

وَمَا لَهُمْ بِهِ مِنْ عِلْمٍ إِنْ يَتَّبِعُونَ إِلَّا الظَّنَّ
وَإِنَّ الظَّنَّ لَا يُغْنِي مِنَ الْحَقِّ شَيْئًا ۝

فَاعْرِضْ عَنْ مَنْ تَوَلَّىٰ هَٰ عَن ذِكْرِنَا وَلَمْ يُرِدْ إِلَّا
الْحَيَاةَ الدُّنْيَا ۝

ذَٰلِكَ مَبْلَغُهُمْ مِنَ الْعِلْمِ إِنَّ رَبَّكَ هُوَ أَعْلَمُ بِمَنْ
صَلَّىٰ عَنْ سَبِيلِهِ ۚ وَهُوَ أَعْلَمُ بِمَنِ اهْتَدَىٰ ۝

وَلِلَّهِ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ لَيَجْزِيَنَّ
الَّذِينَ آمَنُوا بِمَا عَمِلُوا وَيَجْزِيَ الَّذِينَ أَحْسَنُوا
بِالْحَسَنَىٰ ۝

الَّذِينَ يَجْتَنِبُونَ كَبِيرَ الْإِثْمِ وَالْفَوَاحِشَ إِلَّا اللَّمَمَ
إِنَّ رَبَّكَ وَاسِعُ الْمَغْفِرَةِ ۚ هُوَ أَعْلَمُ بِكُمْ إِذْ أَنْشَأَكُمْ
مِّنَ الْأَرْضِ وَإِذْ أَنْتُمْ أَجْنَةٌ فِي بُطُونِ أُمَّهَاتِكُمْ
ۚ فَلَا تُزَكُّوْا أَنْفُسَكُمْ هُوَ أَعْلَمُ بِمَنِ اتَّقَىٰ ۝

أَفَرَأَيْتَ الَّذِي تَوَلَّىٰ ۝

وَأَعْطَىٰ قَلِيلًا وَأَكْثَدَ ۝

أَعِنْدَهُ عِلْمُ الْغَيْبِ فَهَوَّيَرُ ۝

أَمْ لَمْ يُنَبِّأْ بِمَا فِي صُحُفِ مُوسَىٰ ۝

وَأَبْرَاهِيمَ الَّذِي وَفَّىٰ ۝

28. Kuonyesha kuwa kuna madhara makubwa kabisa ya duniani na Akhera katika kufuata dhana tu. Inataka kila unalolisema au kulifuata iwe una ujuzi nalo, kama Qurani yote nzima hii inavyosema. Moja katika hizi ni Aya ya 108 ya Surat Yusuf na Aya ya 36 ya Surat Bani Israil na nyingi nyinginezo, na Hadithi za Mtume. Basi natusijifuatie tu ovyo ovyo. Ilimu ya kweli ni: (a) Mwenyezi Mungu amesema, (katika Qurani); (b) Mtume amesema, (katika Hadithi zake Sahihi).

32. Wanatajwa watu wazuri ni wapi na fadhila za Mwenyezi Mungu katika kuwasamehe vijidhambi visivyodhuru sana na kukataza watu wasijione. Unajua hali yako tu, unayoiona nzuri; hujui ya mwenzako ambayo pengine bora mara chungu nzima kuliko hiyo yako.

38. Kwamba haichukui nafsi dhambi za nafsi nyingine

أَلَا تَنْزُرُ وَإِزْرَةً وَزَّرَ أَخْرَةً ۝

39. Na kwamba mtu hatapata ila yale aliyoyafanya

وَأَنْ تَبْسِلَ لِلنَّاسِ إِلَّا مَا سَعَىٰ ۝

40. Na kwamba amali yake itaonekana.

وَأَنَّ سَعْيَهُ سَوْفَ يُرَىٰ ۝

41. Kisha atalipwa malipo yaliyo kamili

ثُمَّ يُجْزَاهُ الْجَزَاءُ الْأَوْفَىٰ ۝

42. Na kwamba mwisho (wa kila jambo) unarejea kwa Mola wako

وَأَنَّ إِلَىٰ رَبِّكَ الْنتَهَىٰ ۝

43. Na kwamba Yeye ndiy. anayeleta ya kufurahisha na ya kuliza

وَأَنَّهُ هُوَ أَضْحَكَ وَأَبْكَىٰ ۝

44. Na kwamba Yeye ndiye Afishaye na kuhuisha

وَأَنَّهُ هُوَ أَمَاتٌ وَأَحْيَا ۝

45. Na kwamba Yeye ndiye aliyeumba dume na jike (la kila kitu)

وَأَنَّهُ خَلَقَ الرُّوحَيْنِ الذَّكَرَ وَالْأُنثَىٰ ۝

46. Katika mbegu ya uzazi inapomiminwa, (inapotiwa katika fuko la uzazi).

مِنْ تَطْفَةٍ إِذَا تُمْنَىٰ ۝

47. Na kwamba ni juu Yake ufufuo mwingine.

وَأَنَّ عَلَيْهِ النَّشْأَةَ الْأُخْرَىٰ ۝

48. Na kwamba Yeye ndiye Atoaye cha kutosheleza na Atoaye cha ziada.

وَأَنَّهُ هُوَ أَعْنَىٰ وَأَقْنَىٰ ۝

49. Na kwamba Yeye ndiye Mola wa (nyota) ya Shiira (wanayoiabudu. Hiyo imeumbwa na Mwenyezi Mungu kama viumbwa vyengine vyote)

وَأَنَّهُ هُوَ رَبُّ الشَّعَرِ ۝

50. Na kwamba Yeye ndiye aliyewaangamiza Adi wa kwanza

وَأَنَّهُ أَهْلَكَ عَادًا الْأُولَىٰ ۝

51. Na Thamudi; hakumbakisha (hata mmoja)

وَتَمُودًا فَمَا أَبْقَىٰ ۝

52. Na kabla (yao) watu wa Nuhu (aliwaangamiza pia). Na wao walikuwa madhalimu zaidi na waovu zaidi

وَقَوْمَ نُوحٍ مِنْ قَبْلُ إِنَّهُمْ كَانُوا هُمْ أَظْلَمَ وَأَطْغَىٰ ۝

53. Na miji iliyopinduliwa (chini juu), ameipindua (yeye hivyo)

وَالْمُؤْتَفِكَةَ أَهْوَىٰ ۝

54. Vikaifunika (miji hiyo) vilivyoifunika.

فَغَشَّاهَا مَا عَشَىٰ ۝

55. Basi neema gani ya Mola wako Unayoifanyia shaka (ukaona labda si yake)?

فَيَأْتِي الْآءَ رَبِّكَ تَتَمَارَىٰ ۝

43-54. Zinatajwa sifa za Mwenyezi Mungu na nguvu zake. Khalafu katika Aya ya 55 wanaulizwa kuwa pana shaka katika haya? Hapana shaka yoyote. Ni kweli tu hii — nyeupe, haina kiza hata chembe. Na inasemwa katika Aya ya 56 kuwa haya yametajwa hata katika hivyo vitabu vya Mitume wa kale kabisa huko. Aya hii ina tafsiri mbili. Moja ni hiyo tuliyoitaja juu na moja: "Haya ni maonyo miongoni mwa maonyo ya kale kabisa."

56. Huyu (Muhammad) ni Mwonyaji (Mtume) miongoni mwa Waonyaji wa zamani (waliopita).

هَذَا نَذِيرٌ مِنَ الذُّرِّ الْأَوَّلِ ۝

57. Tukio lililo karibu (kutokea kwake) linasogea (Kiama kinasogelea).

أَزَقَّتِ الْأَرْقَةُ ۝

58. Hakuna awezaye kuliondoa isipokuwa Mwenyezi Mungu (akitaka)

لَيْسَ لَهَا مِنْ دُونِ اللَّهِ كَاشِفَةٌ ۝

59. Je! Mnaistaajabia Hadithi hii?

أَفَمِنْ هَذَا الْحَدِيثِ تَعْجَبُونَ ۝

60. Na mnacheka; wala hamlii

وَتَضْحَكُونَ وَلَا تَتَّبِعُونَ ۝


61. Na mmeghafilika tu!

وَأَنْتُمْ سَاهُونَ ۝

62. Basi msujudieni Mwenyezi Mungu na mumuabudu.

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اسْجُدُوا لِلَّهِ وَاعْبُدُوا ۝

59-62. Wanasimangwa wabaya.



Ina Aya 55

SURATUL QAMAR

Ina Makara 2

(Imeteremka Makka)

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa, na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

1. Saa (ya kufika Kiama) imekaribia; na mwezi umepasuka.

2. Na wakiona Muujiza hugeuka upande na kusema: "Uchawi tu (huu wake) unazidi kuendelea!"

3. Ndiyo wamekadhibisha hivi na wamefuata matamania ya nafsi zao. Na kila jambo (la Mwenyezi Mungu) ni lenye kuthubuti.

4. Na kwa yakini zimewajia habari zenye makatazo makubwa

5. (Zenye) Hikima kamili. Lakini maonyo (kwao) hayafai kitu

6. Basi jiepushe nao. Na (wakumbushe) Siku atakapoita muitaji huyo kulendea jambo zito (hilo la Kiama)

7. Macho yao yatainama chini; wanatoka katika makaburi kama kwamba ni nzige waliotawanyika

8. Wanamkimbia muitaji huyo na huku wanasema hao makafiri: "(Siku) hii ni siku ngumu (kabisa)."

9. Kabla yao watu wa Nuhu walikadhibisha nao. Walimkadhibisha mja Wetu na wakasema ni mwendawazimu; na akawa anatolewa maneno makali.

10. Ndipo akamuomba Mola wake (akasema): "Kwa hakika mimi nimeshindwa, basi ninusuru."

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

إِن تَرَبَّتِ السَّاعَةُ وَانْشَقَّ الْقَمَرُ ①

وَأَن يَرَوْا آيَةً يُعْرَضُوا وَيَقُولُوا سِحْرٌ مُّسْتَقَرٌّ ②

وَكَذَّبُوا وَاتَّبَعُوا أَهْوَاءَهُمْ وَكُلَّ أَمْرٍ مُّسْتَقَرٌّ ③

وَلَقَدْ جَاءَهُمْ مِنَ الْأَنْبَاءِ مَا فِيهِ مُرْدَجَرٌ ④

حِكْمَةٌ بَالِغَةٌ فَمَا تُعِنُّ الذُّرُ ⑤

فَقُولْ عَنْهُمْ رِيَوْمَ يَدْعُ الدَّاءُ إِلَى شَيْءٍ ثَكْرٍ ⑥

خُسْعًا أَبْصَارُهُمْ يَخْرُجُونَ مِنَ الْأَجْدَاثِ كَأَنَّهُمْ جَرَادٌ مُّنتَشِرٌ ⑦

مُهِطِعِينَ إِلَى الدَّاءِ يَقُولُ الْكُفْرُ وَهَذَا يَوْمُ عَاسِرٍ ⑧

كَذَّبَتْ قَبْلَهُمْ قَوْمُ نُوحٍ فَكَذَّبُوا عَبْدَنَا وَقَالُوا مَجْنُونٌ وَازْدُجِرَ ⑨

قَدْ عَارَ رَبَّةَ إِلَى مَغْلُوبٍ فَانْتَصِرَ ⑩

1. Yanayotajiwa Sura hii ni sawa sawa na tuliyoyatajia Sura Qaf katika Maelezo ya Aya yake ya 1.

6-8. Baadhi ya vishindo vitakavyotokea siku ya Kiama.

9-42. Analiwazwa Mtume kwa kutajiwa kunusuriwa Mitume wenziwe na kuadhibiwa uma zao.

11. Mara Tukaifungua milango ya mbingu kwa maji yanayomiminika (kwa nguvu kabisa).

فَقَتَحْنَا أَبْوَابَ السَّمَاءِ مِنْهُمُ ۝

12. Na Tukazibubujisha maji chemchem zilizo katika ardhi; na maji (ya juu na chini) yakakutana kwa jambo lililokadiriwa (na Mungu).

وَفَجَّرْنَا الْأَرْضَ عُيُونًا فَالْتَقَى الْمَاءُ عَلَى أَمْرٍ قَدْ قُدِرَ ۝

13. Na Tukamchukua (Nabii Nuhu) katika ile (jahazi) iliyotengenezwa kwa mbao na misumari

وَحَمَلْنَاهُ عَلَى ذَاتِ الْأَوَّاحِ وَدُسُرٍ ۝

14. Ikawa inakwenda mbele ya macho, (hifadhi) Yetu. Hii ni tunzo (tuzo) kwa yule aliyekuwa amekataliwa (amekanushwa).

تَجَرَّيْ بِأَعْيُنِنَا جَزَاءَ لِمَنْ كَانَ كُفِرَ ۝

15. Na kwa yakini Tuliacha iwe alama. Lakini Je, yuko anayekumbuka?

وَلَقَدْ نَزَّلْنَاهَا آيَةً فَهَلْ مِنْ مُدْكِرٍ ۝

16. Basi ilikuwaje adhabu Yangu na maonyo Yangu?

فَكَيْفَ كَانَ عَذَابِي وَنَذِيرٍ ۝

17. Na kwa yakini Tumeifanya Qurani iwe nyepesi kufahamika (ili iwe kikumbusho). Lakini yuko anayekumbuka?

وَلَقَدْ يَسَّرْنَا الْقُرْآنَ لِلذِّكْرِ فَهَلْ مِنْ مُدْكِرٍ ۝

18. Walikadhibisha kina Adi (nao); basi ilikuwaje adhabu Yangu na maonyo Yangu!

كَذَّبَتْ عَادٌ فَكَيْفَ كَانَ عَذَابِي وَنَذِيرٍ ۝

19. Hakika Tuliwapelekea upepo mkali katika siku ya nuhsi iendeleayo (kwao mpaka leo)

إِنَّا أَرْسَلْنَا عَلَيْهِمْ رِيحًا صَرْصَرًا فِي يَوْمٍ نَحْسٍ مُسَوِّدٍ ۝

20. Ukiwang'oa watu (katika ardhi kisha unawabwata chini, wamelala, wamekufa) kana kwamba ni magogo ya mitende iliyong'olewa.

تَنْزِيلُ الْإِنْسَانِ كَأَنَّهُمْ أَجْنَارٌ نَخِيلٌ مُنْقَعِرٍ ۝

21. Basi ilikuwaje adhabu Yangu na maonyo Yangu!

فَكَيْفَ كَانَ عَذَابِي وَنَذِيرٍ ۝

22. Na kwa yakini Tumeifanya Qurani iwe nyepesi kufahamika (ili iwe kikumbusho). Lakini, yuko anayekumbuka?

وَلَقَدْ يَسَّرْنَا الْقُرْآنَ لِلذِّكْرِ فَهَلْ مِنْ مُدْكِرٍ ۝

23. Thamudi (kadhalika) waliwakadhibisha Waonyaji.

كَذَّبَتْ ثَمُودُ بِالنُّذُرِ ۝

24. Wakasema: "Oh! Tumfuate mtu mmoja miongoni mwetu! Kwa hakika tutakuwa katika upotofu (upotevu) na kichaa (wazimu)."

فَقَالُوا أَبَشْرًا مِثْلَا وَاحِدٍ أَنْبِئُهُ إِنَّا إِذَا لَفِئَ صُلْبٍ ۝

25. "Oh! Ameteremshiwa yeye tu ukumbusho (huo — ya kuwa Mwenyezi Mungu ni mmoja) baina yetu sote? Bali yeye ni muongo, (na) mwenye kujiona."

ءَالْفِئَ الذِّكْرِ عَلَيْهِ مِنْ بَيْنِنَا بَلْ هُوَ كَذَّابٌ أَشِرٌّ ۝

15. Vyombo hivi vyote vinavyokwenda baharini vinakumbusha kitendo hicho kilichotokea zama za Nabii Nuhu. Na vile vile kumbukumbu zake zimetajwa katika vitabu vyote vya Mwenyezi Mungu.

26. Watajua kesho ni nani muongo anayejiona.

27. (Tukamwambia Mtume wao) Tutawaletea ngamia jike ili kuwajaribu, basi watazame tu na ustahamili.

28. Na uwajulishe ya kuwa maji (ya nchi hiyo) yatagawanywa baina yao; kila (sehemu ya) maji itahudhuriwa (na yule mwenye zamu vake).

29. Basi (mwisho wake) wakamwita rafiki yao; naye akashika (upanga) akamtumbua (yule ngamia), wakamuua wakamla).

30. Basi ilikuwaje adhabu Yangu na maonyo Yangu!

31. Kwa yakini Tuliwapelekea mngurumo mmoja tu; basi wakawa kama mabuwa ya mwenye kujenga uwa wa mabuwa ukavunjika.

32. Na bila shaka Tumeifanya Qurani iwe nyepesi kufahamika (ili iwe kikumbusho). Lakini yuko anayekumbuka?

33. Watu wa Luti pia waliwakadhibisha Waonyaji.

34. Hakika Sisi Tuliwapelekea vijiwe (vya kuwatoboa tosi zao vikawaangamiza wote) isipokuwa wafuasi wa Luti; Tuliwaokoa karibu na alfajiri

35. Kwa neema iliyotoka Kwetu. Hivyo ndivyo Tuwalipavyo wanaoshukuru.

36. Na kwa hakika yeye aliwaogopesha adhabu yetu; lakini wao waliyatilia shaka, (walikanusha) maonyo yetu.

37. Na walimtaka (awape) wageni wake (ili wawafanye machafu) Tukayapofusha macho yao; (na tukawaambia) "Onjeni adhabu Yangu na maonyo yangu!"

38. Na ili wajia wakati wa asubuhi adhabu jendeleayo (mpaka leo makaburini mwao humo).

39. (Tukawaambia na tunawaambia): "Onjeni adhabu Yangu na maonyo Yangu."

سَيَعْلَمُونَ عَذَابَ الْكَذَّابِ ۝

إِنَّا مُرْسِلُوا النَّافَةِ فَنَنْتَقِمُ لَهُمْ فَارْتَقِبْهُمْ وَاصْطَبِرْ ۝

وَيُنَبِّئُهُم أَنَّ الْمَاءَ قِسْمَةٌ بَيْنَهُمْ كُلُّ شَرْبٍ مُّخْتَصِرٌ ۝

فَنَادَوْا صَاحِبَهُمْ فَتَعَاطَىٰ فَعَقَرَ ۝

كَيْفَ كَانَ عَذَابِي وَنُذْرِي ۝

إِنَّا أَرْسَلْنَا عَلَيْهِمْ صَيْحَةً وَاحِدَةً فَكَانُوا

كَهَشِيمٍ الْمُخْتَطِرِ ۝

وَلَقَدْ يَسَّرْنَا الْقُرْآنَ لِلذِّكْرِ فَهَلْ مِنْ مُّدَكِّرٍ ۝

كَذَّبَتْ قَوْمُ لُوطٍ بِالنُّذْرِ ۝

إِنَّا أَرْسَلْنَا عَلَيْهِمْ حَاصِبًا إِلَّا آلَ لُوطٍ نَّجَّيْنَاهُمْ

بِسَحَرٍ ۝

نَقِمْنَا مِنْ عِنْدِكَ لَكَ أَنْ تَجْزِيَ مَنْ شَكَرَ ۝

وَلَقَدْ أَنْذَرَهُمْ بَطْشَتَنَا فَتَمَارَوْا بِالنُّذْرِ ۝

وَلَقَدْ رَاودُوهُ عَنْ صَيفِهِ فَطَسْنَا أَعْيُنَهُمْ فَذُوقُوا

عَذَابِي وَنُذْرِي ۝

وَلَقَدْ صَبَّحَهُمْ بُكْرَةً عَذَابٌ مُّسْتَقَرٌّ ۝

فَذُوقُوا عَذَابِي وَنُذْرِي ۝

27. Watu hao walimwambia Mtume wao — Nabii Saleh "Kama wewe Mtume lijaalie jabali hili lipasuke, litoke ngamia jike kubwa." Basi akaomba dua, na Mwenyezi Mungu akawapa huo muujiza walioutaka. Lakini waliambiwa "Hamna ruhusa sasa kuteka maji (visimani wala mitoni wala maziwani) kila siku. Siku moja itakuwa zamu yenu ya kuteka na kuyajaza majumbani mwenu, na siku ya pili ni ya kunywa ngamia maji ya mji mzima." Wakakubali sharuti hiyo. Mwisho wakaona taabu, wakamuua.

40. Na bila shaka Tumeifanya Qurani iwe nyepesi kufahamika (ili iwe kikumbusho). Lakini, yuko anayekumbuka?

41. Na waonyaji waliwajia watu wa Firauni (na mwenyewe Firauni)

42. Wakakadhibisha hoja Zetu zote; kwa hivyo Tukawatesa kama anavyotesa Mwenye nguvu, Mwenye uweza.

43. Je! Makafiri wenu ni bora kuliko hao, (kwa hivyo hawataangamizwa?), au yameandikwa vitabuni kwamba nyinyi mtaachwa (hamtaangamizwa kama walivyoangamizwa hao)?

44. Au ndiyo wanasema, "Sisi ni wengi na ni wawezaji kujinusu (basi tutashinda tu)."

45. (Waambie): "Wingi wao huo karibuni hivi utaendeshwa mbio na watageuza migongo (wanakimbizana)."

46. Walakini Kiama ndio wakati wao (khasa walioahidiwa kuadhibiwa). Na saa hiyo ni nzito sana na chungu kabisa.

47. Bila shaka waovu hawa wamo katika upotofu (upotevu) na kichaa (wazimu).

48. (Wakumbushe) Siku watakayokokotwa Motoni kifudufudi, (na huku wanaambiwa): "Onjeni mguso wa Jahanamu."

49. Kwa hakika Sisi Tumekiumba kila kitu kwa kiasi (chake makhsusi).

50. Na hakukuwa (kupitisha) amri Yetu ila ni mara moja (tu hivi) kama kupepesa jicho (kufumba na kufumbua).

51. Na kwa yakini Tumekwishawaangamiza wenzenu; lakini yuko anayekumbuka?

52. Na kila jambo walilofanya limo madaftarini.

53. Na kila kidogo na kikubwa kimeandikwa.

54. Bila shaka wamchao Mwenyezi Mungu watakuwa katika Mabustani na mito

55. Katika makao mazuri katika (Pepo) ya (Mwenyezi Mungu) — Mfalme Mwenye uweza (wa kila kitu).

وَلَقَدْ يَسَّرْنَا الْقُرْآنَ لِلذِّكْرِ فَهَلْ مِنْ مُدَكِّرٍ ۝

وَلَقَدْ جَاءَ آلَ فِرْعَوْنَ التَّنْذِيرُ ۝

كَذَّبُوا بِآيَاتِنَا كُلِّهَا فَأَخَذْنَاهُمْ أَخْذَ عَزِيزٍ مُقْتَدِرٍ ۝

أَكْفَارُكُمْ خَبِيرٌ مِنْ أُولَئِكَ أَمْرُكُمْ بِرَاءَةٌ فِي الزُّبُرِ ۝

أَمْ يَقُولُونَ نَحْنُ جَمِيعٌ مُنْتَصِرٌ ۝

سَيَهْرُمُ أَجْمَعٌ وَيُولَوْنَ الدُّبُرَ ۝

بَلِ السَّاعَةُ مَوْعِدُهُمْ وَالسَّاعَةُ أَذًى وَآمْرٌ ۝

إِنَّ الْمُجْرِمِينَ فِي ضَلَالٍ وَسُعُرٍ ۝

يَوْمَ يُسْحَبُونَ فِي النَّارِ عَلَى وُجُوهِهِمْ ذُوقُوا مَسَّ سَقَرَ ۝

إِنَّا كُلَّ شَيْءٍ خَلَقْنَاهُ بِقَدَرٍ ۝

وَمَا أَمْرُنَا إِلَّا وَاحِدَةٌ كَلَمْحٍ بِالْبَصَرِ ۝

وَلَقَدْ أَهْلَكْنَا أَشْيَاءَكُمْ فَهَلْ مِنْ مُدَكِّرٍ ۝


وَكُلُّ شَيْءٍ نَعْلَمُهُ فِي الزُّبُرِ ۝

وَكُلُّ صَغِيرٍ وَكَبِيرٍ مُسْتَطَرٌ ۝

إِنَّ الْمُتَّقِينَ فِي جَنَّاتٍ وَنَهَرٍ ۝

فِي مَقْعَدٍ صَدِيقٍ عِنْدَ مَلِيكٍ مُقْتَدِرٍ ۝

43-53. Anaambiwa kuwa na maadui zake yatawafika nao, duniani na Akhera kama yatakayowafika hao.



Ina Aya 78

SURATUR RAHMAN

Ina Makara 3

(Imeteremka Madina)

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa, na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

1. (Mwenyezi Mungu) Mwingi wa rehema.
2. Amefundisha Qurani.
3. Amemuumba binadamu
4. Akamfundisha kunena.
5. Jua na mwezi (hwenda) kwa hisabu (yake).
6. Na miti midogo na mikubwa yote inamnyenyekea (Mwenyezi Mungu).
7. Na mbingu Ameziinua juu na Ameweka uadilifu (insafu)
8. Ili msidhulumu katika kupima (na mengineyo).
9. Basi pimeni kipimo kwa haki wala msipunguze mizani.
10. Na ardhi Ameiweka (Ameitandaza) kwa ajili ya viumbe
11. Humo yamo matunda na mitende yenye matumba (mafumba).
12. Na vimo vyakula vilivyo punje punje zenye makapi, na mimea yenye harufu nzuri.
13. Basi nyinyi viumbe namna mbili — (Binadamu na Majini) — ipi katika neema za Mola wenu mnayoikanusha (kuwa si neema yake)?
14. Amemuumba mtu kwa udongo wa ufinyanzi (utoao sauti) kama vyombo vya udongo

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

الرَّحْمَنُ ۝

عَلَّمَ الْقُرْآنَ ۝

خَلَقَ الْإِنْسَانَ ۝

عَلَّمَهُ الْبَيَانَ ۝

الشَّمْسُ وَالْقَمَرُ بِحُسْبَانٍ ۝

وَالنَّجْمُ وَالشَّجَرُ يَسْجُدَانِ ۝

وَالسَّمَاءَ رَفَعَهَا وَوَضَعَ الْمِيزَانَ ۝

أَلَّا تَطْغَوْا فِي الْمِيزَانِ ۝

وَأَقِيمُوا الْوَزْنَ بِالْقِسْطِ وَلَا تُخْسِرُوا الْمِيزَانَ ۝

وَالْأَرْضَ وَضَعَهَا لِلْأَنَامِ ۝

فِيهَا نَارُهَاةٌ وَالنَّخْلُ ذَاتُ الْأَكْمَامِ ۝

وَالْحَبُّ ذُو الْعَصْفِ وَالرَّيْحَانُ ۝

فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبِينَ ۝

خَلَقَ الْإِنْسَانَ مِنْ صَلْصَالٍ كَالْفَخَّارِ ۝

13. Makadiyani Katika hii Aya waliyoifanya kuwa ni ya 14 wametia ukafiri wao tena wa kukataa Majini. Na tumeirejeza itikadi hii katika Aya ya 112 ya *Suratul An-am*.

Na shetani akazidi kuwafedhehesha hapa wakasema: "Lakini kwa dasturi ya Kiarabu maneno wanayoambiwa watu wengi yanapotaka kutiwa mkazo hutamkwa katika jinsi ya uwili." Mwenye akili yake hasemi uwongo huu? Maelezo yake yamo katika Aya ya 29 ya *Suratul Ahqaf*.

15. Na Akawaumba majini kwa ulimi wa moto.
16. Basi ipi katika neema za Mola wenu mnayoikanusha (kuwa si neema yake)?
17. Mola wa mashariki mbili na Mola wa magharibi mbili.
18. Basi ipi katika neema za Mola wenu mnayoikanusha (kuwa si neema yake)?
19. Anazikutanisha bahari mbili (ya maji ya chumvi na ya maji ya tamu)
20. Baina yao kuna kizuwizi, haziingiliani (zikaharibiana kabisa kabisa).
21. Basi ipi katika neema za Mola wenu mnayoikanusha (kuwa si neema yake)?
22. Katika hizo bahari mbili hutoka lulu na marijani.
23. Basi ipi katika neema za Mola wenu mnayoikanusha (kuwa si neema yake)?
24. Na yako katika amri Yake haya yaliyotengenezwa yakawa yanakwenda baharini; utadhani milima.
25. Basi ipi katika neema za Mola wenu mnayoikanusha (kuwa si neema yake)?
26. Kila kilichoko juu yake (ardhi na mbingu) kitatoweka, (kitaondoka).
27. Inabaki dhati ya Mola wako (tu Mwenyewe) Mwenye utukufu na hishima.
28. Basi ipi katika neema za Mola wenu mnayoikanusha (kuwa si neema yake)?
29. Vinamuomba Yeye kila vilivyomo mbinguni na ardhini: kila siku Yeye yumo katika mambo (mengine mengine).
30. Basi ipi katika neema za Mola wenu mnayoikanusha (kuwa si neema yake)?

وَحَلَقَ الْجَانَّ مِنْ مَّارِجٍ مِّنْ نَّارٍ ۝١٥

فِي أَيِّ آيَةٍ رَّبِّكُمَا تَكْذِبِينَ ۝١٦

رَبُّ الْمَشْرِقَيْنِ وَرَبُّ الْمَغْرِبَيْنِ ۝١٧

فِي أَيِّ آيَةٍ رَّبِّكُمَا تَكْذِبِينَ ۝١٨

مَرَجَ الْبَحْرَيْنِ يَلْتَقِيَانِ ۝١٩

بَيْنَهُمَا بَرْزَخٌ لَا يَبْغِيَانِ ۝٢٠

فِي أَيِّ آيَةٍ رَّبِّكُمَا تَكْذِبِينَ ۝٢١

يَخْرُجُ مِنْهُمَا اللُّؤْلُؤُ وَالْمَرْجَانُ ۝٢٢

فِي أَيِّ آيَةٍ رَّبِّكُمَا تَكْذِبِينَ ۝٢٣

وَلَهُ الْجَوَارِ الْمُنشَآتُ فِي الْبَحْرِ كَالْأَعْلَامِ ۝٢٤

فِي أَيِّ آيَةٍ رَّبِّكُمَا تَكْذِبِينَ ۝٢٥

كُلٌّ مِّنْ عَلَيْهَا فَإِنَّ ۝٢٦

وَيَبْقَى وَجْهُ رَبِّكَ ذُو الْجَلَالِ وَالْإِكْرَامِ ۝٢٧

فِي أَيِّ آيَةٍ رَّبِّكُمَا تَكْذِبِينَ ۝٢٨

يَسْأَلُهُ مَنْ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ كُلَّ يَوْمٍ ۝٢٩

هُوَ فِي شَأْنٍ ۝٣٠

فِي أَيِّ آيَةٍ رَّبِّكُمَا تَكْذِبِينَ ۝٣١

17. Muradi wa Magharibi mbili na Mashariki mbili ni namna linavyokhitafu jua — katika kuchomoza na kuchwa — katika siku za joto, (Summer) na siku za baridi, (Winter). Na kuonyesha kuwa Mwenyezi Mungu ni huyu huyu mmoja. Lakini kwa maslahi yetu — viumbe vyake — ndiyo maana wakati fulani akafanya hivi na wakati fulani mwingine akafanya hivyo.

19. Katika Aya hii waliyoifanya ya 20 wametia farumu za uwongo. Bahari hizo ni bahari zote za maji ya chumvi na ya baridi: haikukhusu Mediterranean wala ...

20. Maji ya Mito na ya Bahari yanapokutana yanaharibiana pale pale mwanzo tu, tena juu juu tu.

31. Karibuni hivi tutakukusudieni (kukuhisabuni) enyi majeshi mawili (Wanaadamu na Majini).

32. Basi ipi katika neema za Mola wenu mnayoikanusha (kuwa si neema yake)?

33. Enyi jamii ya majini na watu! Kama mtaweza kupenya katika mbingu na ardhi (ili mkimbie nisikupatani), basi penyeni (nikuoneni)! Hamtapenya ila kwa nguvu (zangu. Nikikupeni nguvu hizo mtaweza).

34. Basi ipi katika neema za Mola wenu mnayoikanusha (kuwa si neema yake)?

35. Mtaletewa muwako wa moto na shaba (iliyoyayushwa); wala nyinyi hamtaweza kujilinda navyo.

36. Basi ipi katika neema za Mola wenu mnayoikanusha (kuwa si neema yake)?

37. Kumbukeni zitakapopasuka mbingu zikawa nyekundu kama ngozi nyekundu.

38. Basi ipi katika neema za Mola wenu mnayoikanusha (kuwa si neema yake)?

39. Siku hiyo hataulizwa kwa dhambi zake mtu wala jini. (Mwenyezi Mungu anajua kila kitu).

40. Basi ipi katika neema za Mola wenu mnayoikanusha (kuwa si neema yake)?

41. Watajulikana waovu kwa alama zao; basi watakatwa kwa nywele za utosi (wao) na kwa miguu (watiwe Motoni).

42. Basi ipi katika neema za Mola wenu mnayoikanusha (kuwa si neema yake)?

43. Hii ndiyo Jahanamu ambayo waovu wakiikadhibisha.

44. Watakuwa wakizunguka baina ya (jahanamu) hiyo na baina ya maji ya moto yachemkayo.

45. Basi ipi katika neema za Mola wenu mnayoikanusha (kuwa si neema yake)?

46. Na mwenye kuogopa kusimamishwa mbele ya Mola wake atapata mabustani (Pepo) mawili.

47. Basi ipi katika neema za Mola wenu mnayoikanusha (kuwa si neema yake)?

سَنَقَرُكُمْ أَيُّهُ الثَّقَلَيْنِ ۝

فَيَأْتِي الْآءَ رَبِّكُمَا تُكَذِّبِينَ ۝

يَبْعَثُ الرَّجِلَ وَالْإِنْسَ إِنِ اسْتَطَعْتُمْ أَنْ تَنْفُذُوا مِنْ أَقْطَارِ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ فَانْفُذُوا لَا تَنْفُذُونَ إِلَّا بِسُلْطَانٍ ۝

فَيَأْتِي الْآءَ رَبِّكُمَا تُكَذِّبِينَ ۝

يُرْسِلُ عَلَيْكُمَا شَوَاطِئَ مِمَّنْ تَارَدَ وَتُحَاسُّ فَلَا تَنْتَصِرِينَ ۝

فَيَأْتِي الْآءَ رَبِّكُمَا تُكَذِّبِينَ ۝

فَإِذَا انشَقَّتِ السَّمَاءُ فَكَانَتْ وَرْدَةً كَالدِّهَانِ ۝

فَيَأْتِي الْآءَ رَبِّكُمَا تُكَذِّبِينَ ۝

فَيَوْمَئِذٍ لَا يُنْفِلُ عَنْ ذِيْبِهِ إِنْسٌ وَلَا جَانٌّ ۝

فَيَأْتِي الْآءَ رَبِّكُمَا تُكَذِّبِينَ ۝

يَعْرِفُ الْمُجْرِمُونَ يَوْمَهُمْ فَيُوْخَذُ بِالْوِصَى وَالْأَقْدَامِ ۝

فَيَأْتِي الْآءَ رَبِّكُمَا تُكَذِّبِينَ ۝

هَذِهِ جَهَنَّمُ الَّتِي يُكَذِّبُ بِهَا الْمُجْرِمُونَ ۝

يُطَوَّفُونَ فِيهَا وَبَيْنَ حَبِيمٍ إِنْ ۝

فَيَأْتِي الْآءَ رَبِّكُمَا تُكَذِّبِينَ ۝

وَلِمَنْ خَافَ مَقَامَ رَبِّهِ جَنَّاتٌ ۝

فَيَأْتِي الْآءَ رَبِّكُمَا تُكَذِّبِينَ ۝

46. Ana Pepo kwa ajili ya kufanya mema na ana Pepo nyingine kwa ajili ya kujiepusha na mabaya.

48. (Mabustani) yenye miti yenye matawi mengi.

49. Basi ipi katika neema za Mola wenu mnayoikanusha (kuwa si neema yake)?

50. Ndani yake zimo chemchem mbili zinapita (kwa vizuri).

51. Basi ipi katika neema za Mola wenu mnayoikanusha, (kuwa si neema yake)?

52. Muna humo, katika kila matunda, namna mbili (na zaidi za kila aina).

53. Basi ipi katika neema za Mola wenu mnayoikanusha, (kuwa si neema yake)?

54. Wawe Wameegemea kwenye matandiko ambayo bitana zake (vitambaa vyake vya ndani) ni za hariri nzito; na matunda ya Mabustani hayo yananing'inia, (mepesi kuchumika).

55. Basi ipi katika neema za Mola wenu mnayoikanusha, (kuwa si neema yake)?

56. Watakuwamo humo wanawake watulizao macho yao; binadamu yoyote hajawagusa kabla yao (hao waume wao) wala jini.

57. Basi ipi katika neema za Mola wenu mnayoikanusha, (kuwa si neema yake)?

58. Kama kwamba wao (wanawake hao) ni yakuti na marijani.

59. Basi ipi katika neema za Mola wenu mnayoikanusha, (kuwa si neema yake)?

60. Hakuna malipo ya ihsani ila kulipa ihsani (vile vile).

61. Basi ipi katika neema za Mola wenu mnayoikanusha, (kuwa si neema yake)?

62. Na zaidi ya hizo yako Mabustani mawili mengine.

63. Basi ipi katika neema za Mola wenu mnayoikanusha, (kuwa si neema yake)?

64. Yenye rangi nzuri ya kijani kilichowiva (bara bara).

65. Basi ipi katika neema za Mola wenu mnayoikanusha, (kuwa si neema yake)?

ذَوَاتَا أَفْنَانٍ ۝

فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبِينَ ۝

فِيهِمَا عَيْنَيْنِ تَجْرِينَ ۝

فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبِينَ ۝

فِيهِمَا مِنْ كُلِّ فَاكِهَةٍ زَوْجِينَ ۝

فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبِينَ ۝

مُتَكِّينَ عَلَى فُرُشٍ بَطَائِنُهَا مِنْ إِسْتَبْرَقٍ ۝

وَجَنَّاتٍ أَلْفَافٍ ۝

فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبِينَ ۝

فِيهِنَّ قُصُورٌ مِثْلُ الطَّرَفِ، لَمْ يَطْمِثْهُنَّ إِنْسٌ

قَبْلَهُمْ وَلَا جَانٌ ۝

فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبِينَ ۝

كَأَنَّهُنَّ الْيَاقُوتُ وَالْمَرْجَانُ ۝

فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبِينَ ۝

هَلْ جَزَاءُ الْإِحْسَانِ إِلَّا الْإِحْسَانُ ۝

فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبِينَ ۝

وَمِنْ دُونِهِمَا جَنَّتَيْنِ ۝

فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبِينَ ۝

مُدْهَامَتَيْنِ ۝

فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبِينَ ۝

56. Wake zetu hawa hawa wa kilimwenguni wataumbwa upya kama vile awali kabla hawajagusa na yoyote; na waume zao watakuwa wapya nao vile vile na hirimu moja, kama ilivyo katika Aya ya 37 ya *Suratul Waaqiah*.

66. Muna humo chemchem mbili zinazofoka (maji kwa nguvu).

فِيهَا عَيْنٌ نَضَّاحَتَيْنِ ۝

67. Basi ipi katika neema za Mola wenu mnayoikanusha, (kuwa si neema yake)?

فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبِينَ ۝

68. Imo humo (miti ya) matunda (ya kila namna) na (hasa) mitende na mikomamanga.

فِيهَا فَاكِهَةٌ وَنَخْلٌ وَرُمَّانٌ ۝

69. Basi ipi katika neema za Mola wenu mnayoikanusha (kuwa si neema yake)?

فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبِينَ ۝

70. Wamo humo wanawake wazuri (wa tabia), wazuri (wa sura pia).

فِيهِنَّ خَيْرَاتٌ حِسَانٌ ۝

71. Basi ipi katika neema za Mola wenu mnayoikanusha, (kuwa si neema yake)?

فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبِينَ ۝

72. Wenye macho meupe mazuri makubwa, wanao:awishwa majumbani.

حُورٌ مَّقْصُورَاتٌ فِي الْبُحَيْرِ ۝

73. Basi ipi katika neema za Mola wenu mnayoikanusha, (kuwa si neema yake)?

فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبِينَ ۝

74. Hajawagusa binadamu yoyote kabla yao (hao waume zao) wala jini.

لَمْ يَطِئْتُهُنَّ اِنْسٌ قَبْلَهُمْ وَلَا جَانٌ ۝

75. Basi ipi katika neema za Mola wenu mnayoikanusha, (kuwa si neema yake)?

فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبِينَ ۝

76. Wategemee matakia ya kijani kibichi na (wakae) juu ya mazulia mazuri.

مُتَكِينِينَ عَلَى رُفُوفٍ خُضِرَ وَعْبَقَرِيٍّ ۝

77. Basi ipi katika neema za Mola wenu mnayoikanusha, (kuwa si neema yake)?

فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبِينَ ۝

78. Limetukuka jina la Mola wako Mwenye utukufu na hishima.

يَا تَبَرَّكَ اسْمُ رَبِّكَ ذِي الْجَلَالِ وَالْإِكْرَامِ ۝



Ina Aya 96

SURATUL WAQIAH

Ina Makara 3

(Imeteremka Makka)

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuncemesha neema kubwa kubwa, na Mwenye kuncemesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

1. (Wakumbushe) Litakapotokea tokeo (hilo la Kiyama)

إِذَا وَقَعَتِ الْوَاقِعَةُ ۝

2. Ambalo Kutokea kwake si uwongo.

لَيْسَ لَوْفَعَتِهَا كَاذِبَةٌ ۝

3. Lifedheheshalo (wabaya), litukuzalo (wazuri)

خَافِضَةٌ رَّافِعَةٌ ۝

4. Ardhi itakapotetemeshwa mtetemesho mkubwa

إِذَا رُجَّتِ الْأَرْضُ رَجًا ۝

5. Na milima itakaposagwasagwa

وَبُسَّتِ الْجِبَالُ بَسًا ۝

6. Iwe mavumbi yanayopeperushwa

فَكَانَتْ هَبَاءً مُنْبَثًا ۝

7. Na nyinyi mtakuwa namna tatu.

وَكُنْتُمْ أَزْوَاجًا ثَلَاثَةً ۝

8. Watu wenye kheri; watakuwa namna gani hawa watu wenye kheri!

فَأَصْحَبُ الْمُيْمَنَةِ ۝ مَا أَصْحَبُ الْمُيْمَنَةِ ۝

9. Na watu wenye shari; watakuwa namna gani hawa watu wenye shari!

وَأَصْحَبُ الشُّمَلَةِ ۝ مَا أَصْحَبُ الشُّمَلَةِ ۝

10. Na walioko mbele (kabisa katika heri) nao ndio walioko mbele

وَالشُّقُونَ الشُّقُونَ ۝

11. Hao ndio watakaokaribishwa (kwa Mwenyezi Mungu)

أُولَئِكَ الْمُقَرَّبُونَ ۝

12. Katika Mabustani yenye neema.

فِي جَنَّاتِ النَّعِيمِ ۝

13. Sehemu kubwa (katika hawa) ni miongoni mwa (watu) wa mwanzo (huko)

ثَلَاثٌ مِّنَ الْأَوَّلِينَ ۝

14. Na Sehemu ndogo ni miongoni mwa (watu) wa mwisho, (Huu umma wa Nabii Muhammad).

وَقَلِيلٌ مِّنَ الْآخِرِينَ ۝

15. Watakuwa juu ya viti vya fahari vilivyotonewa, (vilivyotiwa mapambo)

عَلَى سُرُرٍ مَّوْضُونَةٍ ۝

13. Wamekuwa wao wengi katika hiyo Daraja ya Assabiquna kwa kuwa hiyo ndiyo daraja ya Mitume na wale walio safi kabisa kabisa. Na uma wetu huu tunaye Mtume wetu mmoja tu na wale wasafiwa wake waliosafiwa kabisa. Basi wametushinda kwa idadi.

Ama katika Daraja ya As-habul Yamin sisi uma mmoja tumekuwa sawa sawa na uma zote hizo.

16. Wataviegemea waelekeane (wanazungumza).
 17. Wawe wanawazungukia wavulana, (watumishi watoto wanaume) walio daima na sura za ujana za kupendeza
 18. Kwa vikombe na mabirika, na gilasi za Vinywaji vinavyotoka katika mito inayoonekana mapitio yake
 19. Hawataumwa na vichwa kwa (kuvinywa vinywaji) hivyo wala hawatatokwa na akili
 20. Na matunda (namna kwa namna) kama watakayopenda
 21. Na nyama za ndege kama watakavyotamani (wenyewe).
 22. Na wanawake wenye macho mazuri na makubwa, (ya vikombe)
 23. (Wanapendeza na safi) kama kwamba ni lulu zilizofichwa (katika machaza yake, ndio kwanza zinapasuliwa).
 24. Ni jaza ya hayo waliyokuwa wakiyatenda.
 25. Hawatasikia humo maneno ya upuuzi wala maneno ya dhambi
 26. Isipokuwa maneno ya salama na amani.
 27. Na wale watu wa kheri nao; watakuwa namna gani watu hao wa kheri!
 28. (Watakuwa) katika (vivuli vya) mikunazi isiyo na miba
 29. Na migomba iliyopangiliwa (uzuri na iliyopangilika) mazao (yake vizuri)
 30. Na (katika) vivuli (vyengine) vilivyonyoka (kila upande)
 31. Na maji yanayomiminika (kwa vizuri)
 32. Na matunda mengi (ya kila namna)
 33. Hayatindiki (hayakomi) wala hayakatazwi (kwa kuwa si yake huyu au yanamdhuru)
 34. Na Wanawake watukufu; (hawa waliokuwa nao duniani).
 35. Tutawaumba kwa umbo (bora zaidi)
- مُنْكِبِينَ عَلَيْهَا مُتَقِِّلِينَ ۝
 يُطَوَّفُ عَلَيْهِمْ وَلَدَانُ مُخَلَّدُونَ ۝
 بِأَكْوَابٍ وَأَبَارِيقَ زَكَوَاتٍ مِنْ مَّعِينٍ ۝
 لَا يُصَدَّعُونَ عَنْهَا وَلَا يُنْفَوْنَ ۝
 وَفَاكِهَةً مِمَّا يَتَخَبَّرُونَ ۝
 وَلَحْمَ طَيْرٍ مِمَّا يَشْتَهُونَ ۝
 وَخَوْرَ عَيْنٍ ۝
 كَأَمْثَالِ اللُّؤْلُؤِ الْمَكْنُونِ ۝
 جَزَاءُ بِمَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ۝
 لَا يَسْمَعُونَ فِيهَا لَغْوًا وَلَا تَأْثِيمًا ۝
 إِلَّا قِيلًا سَلَامًا سَلَامًا ۝
 وَأَصْحَابُ الْيَمِينِ هَٰذَا أَصْحَابُ الْيَمِينِ ۝
 فِي سِدْرٍ مَخْضُودٍ ۝
 وَطَلْحٍ مَّنْضُودٍ ۝
 وَظِلٍّ مَّمْدُودٍ ۝
 وَمَاءٍ مَّسْكُوبٍ ۝
 وَفَاكِهَةٍ كَثِيرَةٍ ۝
 لَا مَقْطُوعَةٍ وَلَا مَمْنُوعَةٍ ۝
 وَفُرُشٍ مَّرْفُوعَةٍ ۝
 إِنَّا أَنشَأْنَهُمْ إِنشَاءً ۝

36. Na Tutawafanya vijana kama kwamba ndio kwanza wanaolewa

فَجَعَلْنَهُنَّ أَبْكَارًا ۝

37. Wanapendana na waume zao (walio) hirimu moja na wao

عُرَبًا أَتْرَابًا ۝

38. (Yote haya yatafanywa) kwa ajili ya watu wa kheri.

لَا صَاحِبَ الْيَمِينِ ۝

39. Sehemu kubwa (katika hawa watu wa kheri) ni miongoni mwa (watu) wa (uma za) mwanzo

ثُلَّةٌ مِنَ الْأَوَّلِينَ ۝

40. Na sehemu kubwa (pia) ni miongoni mwa (watu) wa mwisho (wa huu uma wa Nabii Muhammad).

وَسُلَّةٌ مِنَ الْآخِرِينَ ۝

41. Na watu wa shari (waovu); watakuwa namna gani hao watu wa shari!

وَأَصْحَابُ الشَّالِ ۝ مَا أَصْحَابُ الشَّالِ ۝

42. (Watakuwa) katika upepo wa Moto na maji yachemkayo

فِي سُومٍ وَحَمِيمٍ ۝

43. Na kivuli cha moshi mweusi sana

وَذِلٍّ مِّنْ يَحْمُومٍ ۝

44. Si cha (kuleta) baridi wala si cha starehe.

لَا بَارِدٍ وَلَا كَرِيمٍ ۝

45. Bila shaka wao walikuwa kabla ya haya wakiishi maisha ya anasa.

إِنَّمَا كَانُوا قَبْلَ ذَلِكَ مُتْرَفِينَ ۝

46. Na walikuwa wakishikilia (wakiendelea) (kufanya) madhambi makubwa.

وَكَانُوا يُصْرُونَ عَلَى الْيَحْتِ الْعَظِيمِ ۝

47. Na walikuwa wakisema: "Tutakapokufa na tukawa udongo na mifupa, ndio tutafufuliwa? (Ni uwongo huo)

وَكَانُوا يَقُولُونَ ۝ إِذَا مِتْنَا وَكُنَّا تُرَابًا

وَعِظَامًا ۝ إِنَّا لَبَعُوثُونَ ۝

48. "Au wazee wetu wa zamani (ndio watafufuliwa pia)?"

أَوِ آبَاؤُنَا الْأَوَّلُونَ ۝

49. Sema: "Bila shaka wa kwanza na wa mwisho"

قُلْ إِنَّ الْأَوَّلِينَ وَالْآخِرِينَ ۝

50. "Watakusanywa kwa wakati (uliowekwa) katika siku maalumu."

لَجُجُوعُونَ ۝ إِلَىٰ مِيقَاتِ يَوْمٍ مَّعْلُومٍ ۝

51. "Kisha nyinyi, mliopotea (na) kukadhibisha,"

ثُمَّ إِنَّكُمْ أَنتُمُ الصَّاكُونَ الْمَكْدُوبُونَ ۝

52. "Kwa yakini mtakula mti wa Mzakkum;"

لَا يَكُونُ مِنْ شَجَرٍ مِّنْ زُقُومٍ ۝

37. Hapo Peponi watakuwa watu wote umri mmoja, waliokufa watu wazima na waliokufa vijana, waume na wanawake. Wote watakuwa katika umri kamili wa ujana.

52. Makadiyani Katika Aya hii waliyofanya ya 53 wametia ushetani wao wa kuukataa *Mshajaratuz Zaqqum* kama walivyofanya katika Aya ya 62 ya *Surat Wassaaffaat*. Na tumewajibu.

52-54. Kama zilivyotajwa neema watakazozipata watu wema basi hapa inatajwa nakama itakayowapata waovu.

53. "Na kwa huo mtajaza matumbo (yenu)."
54. "Na juu yake mtakunywa maji ya moto yanayochemka."
55. "Tena mtakunywa kama wanywavyo ngamia wenye kiu sana, (na kila wakinywa kiu haiweshi)."
56. Hiyo ni karamu yao siku ya malipo.
57. Sisi tumekuumbeni, basi hamsadiki (kuwa tunaweza kukurejesheni?)
58. Je! Mnaiona mbegu ya uzazi mnayoitoneza, (mnayoidondokeza).
59. Je, mnaiumba nyinyi (ikawa kiumbe) au Tunaiumba Sisi?"
60. Sisi Tumekuwekeeni mauti; basi hatutashindwa (kukufufueni wala)
61. (Hatutashindwa) kuwaleta wengine badala yenu na kukuumbeni nyinyi katika umbo (jingine lisilikuwa la Kibinadamu), msilolijua.
62. Na bila shaka nyinyi mnajua umbo la kwanza (hili walilionalo viumbe wote), (kuwa tumelifanya sisi); kwa nini hamkumbuki (basi kuwa sisi ni waweza vile vile wa hilo umbo la pili).
63. Je! Mnaiona mimea mnayoipanda?
64. Je! Mnaiotesha nyinyi au Sisi ndiyo tunayoioresha?
65. Tungalitaka Tungaliifanya mapepe — (haizai), mkawa mnanung'unika tu.
66. (Mkawa Mnasema): "Hakika sisi tumegharimika bure."
67. "Bali sisi tumenyimwa (faida ya jitihada tuliopitisha)."
68. Je! Mnayaona maji ambayo mnayanywa?
69. Je! Mumeyateremsha nyinyi mawinguni au Sisi ndio tunaoyateremsha?

فَمَا لُتُونَ مِنْهَا الْبُطُونَ ۖ
فَشْرَبُونَ عَلَيْهِ مِنَ الْحَمِيمِ ۖ
فَشْرَبُونَ شَرْبَ الْهَيْمِ ۖ

هَذَا نُزْلُهُمْ يَوْمَ الدِّينِ ۖ
نَحْنُ خَلَقْنَكُمْ فَلَوْلَا تَصَدَّقُونَ ۖ

أَفَرَأَيْتُمْ مَا تُمْنُونَ ۖ

ءَأَنْتُمْ تَخْلُقُونَهَا أَمْ نَحْنُ الْخَالِقُونَ ۖ
نَحْنُ قَدَرْنَا بَيْنَكُمْ الْمَوْتَ وَمَا نَحْنُ
بِمُسْبِقِينَ ۖ

عَلَى أَنْ تُبَدِّلَ أَمْثَالَكُمْ وَتُنْشِئَكُمْ فِي مَا لَا
تَعْلَمُونَ ۖ

وَلَقَدْ عَلِمْتُمُ النَّشْأَةَ الْأُولَىٰ فَلَوْلَا تَذَكَّرُونَ ۖ

أَفَرَأَيْتُمْ مَا تَحْرُثُونَ ۖ
ءَأَنْتُمْ تَزْرَعُونَهَا أَمْ نَحْنُ الزَّارِعُونَ ۖ

لَوْ شَاءَ لَجَعَلْنَاهُ حُطًا مَّا فَطَلْتُمْ تَفَكَّهُونَ ۖ

إِنَّا لَمُعَرِّمُونَ ۖ

بَلْ نَحْنُ مَحْرُومُونَ ۖ

أَفَرَأَيْتُمُ الْمَاءَ الَّذِي تَشْرَبُونَ ۖ
ءَأَنْتُمْ أَنْزَلْتُمُوهُ مِنَ الْمُزْنِ أَمْ نَحْنُ الْمُنْزِلُونَ ۖ

58-73. Tunatajiwa baadhi ya neema alizotufanyia. Na baada ya kila moja anatwambia: "Mumejifanyia nyinyi haya au Mimi (Mwenye enzi Mungu) ndiye niliyekufanyieni?" Basi tunaposoma kila moja katika suala hizi tuseme "Bal Anta Rabbuna Falakal Hamd" (Bali ni wewe Mola wetu, basi tunakushukuru).

70. Tungalitaka Tungaliyafanya ya chumvi, (makali). Basi mbona hamshukuru?

71. Je! Mnauona moto ambao mnauasha?

72. Je! Mti wake mumeuumba nyinyi au Sisi ndio tuliouumba?

73. Sisi Tumeufanya kuwa ukumbusho (wa moto wa Akhera) na manufaa kwa viumbe.

74. Basi litukuze jina la Mola wako Aliye Mkuu.

75. Basi Ninaapa kwa maanguko ya nyota, (kwa kuchwa nyota)

76. Na hakika hicho bila shaka ni kiapo kikubwa, laiti mngalijua!

77. Bila shaka hiki (mnachosomewa) ni Kitabu kilichokusanya kila yanayohitajiwa na Chenye hishima

78. Kilichotolewa katika hicho Kitabu kilichohifadhiwa kweli kweli, (*Lawhul Mahfudh*).

79. Hapana akigusaye ila waliotakaswa na mabaya.

80. Ni uteremsho unaotoka kwa Mola wa walimwengu.

81. Je! Mnaibeza Hadithi hii? (Mnayapuuza yaliyo katika Kitabu hiki?)

82. Na mnafanya kuikadhibisha ndiyo (shukrani ya) pato lenu (alilokuruzukuni)?

83. Basi mbona (roho) ifikapo kooni

84. Na nyinyi wakati ule mnatazama

85. Nasi Tunakaribiana naye zaidi (huyo anayetoka roho) kuliko nyinyi, wala nyinyi hamuoni.

86. Kama nyinyi hamumo katika mamlaka (yangu)

87. Kwa nini hamuirudishi (hiyo roho), ikiwa mnasema kweli (kuwa hamumo katika mamlaka yangu).

88. Basi akiwa (mtu huyo anayekufa) ni miongoni mwa wale waliokaribishwa (na Mwenyezi Mungu)

لَوْ شَاءَ جَعَلْنَاهُ أَجَاًا فَلَوْلَا تَشْكُرُونَ ۝

أَفَرَأَيْتُمُ النَّارَ الَّتِي تُورُونَ ۝
مَا أَنتُمْ أَنشَأْتُمْ شَجَرَتَهَا أَمْ نَحْنُ الْمُنشِئُونَ ۝

نَحْنُ جَعَلْنَاهَا تَذْكِرَةً وَمَتَاعًا لِّلْمُقْوِينَ ۝

فَسَبِّحْ بِحَمْدِ رَبِّكَ الْعَظِيمِ ۝

فَلَا أُقْسِمُ بِمَوْقِعِ الشُّجُومِ ۝

وَأِنَّهُ لَقَسَمٌ لِّو تَعْلَمُونَ عَظِيمٌ ۝

إِنَّهُ لَقُرْآنٌ كَرِيمٌ ۝

فِي كِتَابٍ مُّكْتُونٍ ۝

لَّا يَشْعُكُ إِلَّا الْمُنْظَرُونَ ۝

تَنْزِيلٌ مِّن رَّبِّ الْعَالَمِينَ ۝

أَفِيهِذَا الْحَدِيثِ أَنتُمْ مُدْهُنُونَ ۝

وَتَجْعَلُونَ رِزْقَكُمْ أَكْكُمْ مُّكَدِّبُونَ ۝

فَلَوْلَا إِذَا بَلَغَتِ الْخُلُقُومَ ۝

وَأَنتُمْ حِينِيذٍ تَنْظُرُونَ ۝

وَنَحْنُ أَقْرَبُ إِلَيْهِ مِنْكُمْ وَلَكِنْ لَا تُبْصِرُونَ ۝

فَلَوْلَا إِنْ كُنْتُمْ غَيْرَ مَدِينِينَ ۝

تَرْجِعُونَهَا إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ ۝

فَأَمَّا إِنْ كَانَ مِنَ الْمُقَرَّبِينَ ۝

89. Basi ni raha (kubwa) na manukato (mazuri) na Mabustani yenye neema (zinamngoja).

فَرَوْحٌ وَرَيْحَانٌ وَجَنَّتْ نَعِيمٌ ﴿٨٩﴾

90. Na kama akiwa ni miongoni mwa watu wa kheri

وَأَمَّا إِن كَانَ مِنْ أَصْحَابِ الْيَمِينِ ﴿٩٠﴾

91. Basi ataambiwa "Ni salama kwako (daima), (uliye) miongoni mwa watu wa kheri."

فَسَلَامٌ لَّكَ مِنْ أَصْحَابِ الْيَمِينِ ﴿٩١﴾

92. Na kama akiwa ni miongoni mwa waliokadhibisha, wapotofu (wapotevu)

وَأَمَّا إِن كَانَ مِنَ الْمَكْدُورِينَ الصَّالِّينَ ﴿٩٢﴾

93. Basi karamu (yake) ni maji ya moto yachemkayo

فَنَزَلَ مِنْ حَمِيمٍ ﴿٩٣﴾

94. Na kuwaka Motoni.


وَتَصْلِيَةٌ جَعِيمٍ ﴿٩٤﴾

95. Bila shaka hii ndiyo haki yenye yakini.

إِنَّ هَذَا لَهُوَ حَقُّ الْيَقِينِ ﴿٩٥﴾

96. Basi litukuze jina la Mola wako mwenye utukufu.

بِجَ فَسَبِّحْ بِاسْمِ رَبِّكَ الْعَظِيمِ ﴿٩٦﴾



Ina Aya 29

SURATUL HADYD

Ina Makara 4

(Imeteremka Madina)

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

1. Kinamtukuza Mwenyezi Mungu kila kilichomo mbinguni na ardhini, na Yeye ndiye Mwenye nguvu, Mwenye hikima.

2. Ufalme wa mbingu na ardhi ni Wake; Anahuisha na Kufisha. Na Yeye ni Mwenye uweza juu ya kila kitu.

3. Yeye ndiye wa Mwanzo na ndiye wa Mwisho, naye ndiye wa Dhahiri na wa Siri, naye ndiye Mjuzi wa kila kitu.

4. Yeye ndiye Aliyeziumba mbingu na ardhi katika nyakati sita; kisha akakaa katika enzi (yake). Anayajua yanayoingia katika ardhi na yanayotoka humo, na yanayoteremka kutoka mbinguni na yanayopanda humo; Naye Yu pamoja nanyi popote mulipo. Na Mwenyezi Mungu Anaona mnayoyatenda (yote).

5. Ufalme wa mbingu na ardhi ni Wake. Na mambo yote yanarudishwa kwa Mwenyezi Mungu.

6. Anaingiza usiku katika mchana na Anaingiza mchana katika usiku. Na Yeye Anajua yaliyomo vifuani, (seuze yanayosemwa au kufanywa).

7. Muaminini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, na toeni katika yale Aliyokupeni. Basi wale walioamini miongoni mwenu na wakatoa, wana malipo makubwa.

8. Na mumekuwa je, hamuamini Mwenyezi Mungu! Na (hali yakuwa) Mtume anakwiteni

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

سَبَّحَ لِلَّهِ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ، وَهُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ①

لَهُ مُلْكُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ، يُحْيِي وَيُمِيتُ، وَهُوَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ②

هُوَ الْأَوَّلُ وَالْآخِرُ وَالظَّاهِرُ وَالْبَاطِنُ، وَهُوَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ③

هُوَ الَّذِي خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ، فِي سِتَّةِ أَيَّامٍ ثُمَّ اسْتَوَى عَلَى الْعَرْشِ، يَعْلَمُ مَا يَلِجُ فِي الْأَرْضِ وَمَا يَخْرُجُ مِنْهَا وَمَا يَنْزِلُ مِنَ السَّمَاءِ وَمَا يَعْرُجُ فِيهَا، وَهُوَ مَعَكُمْ أَيْنَ مَا كُنْتُمْ، وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرٌ ④

لَهُ مُلْكُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ، وَإِلَى اللَّهِ تُرْجَعُ الْأُمُورُ ⑤

يُولِجُ اللَّيْلَ فِي النَّهَارِ وَيُولِجُ النَّهَارَ فِي اللَّيْلِ، وَهُوَ عَلِيمٌ بِذَاتِ الصُّدُورِ ⑥

آمِنُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ وَأَنْقَضُوا مِمَّا جَعَلَكُمْ مُتَخَلِّفِينَ فِيهِ، قَالِ الَّذِينَ آمَنُوا مِنْكُمْ وَأَنْقَضُوا لَهُمْ أَجْرٌ كَبِيرٌ ⑦

وَمَا لَكُمْ لَا تُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالرَّسُولِ، يَدْعُوكُمْ

1-6. Aya za Mwanzo wa Sura hii — kama za mwisho wa *Suratul Hashr* — zinataja nyingi katika sifa za Mwenyezi Mungu. Na watu wanashughulikia kuzisoma hizo za *Suratul Hashr* kuliko hizi; na zote ni sifa za Mungu na zote zimejiwa na Hadithi za kutaja fadhila zake.

7. Haya mali waliyopewa matajiri siyo yawe yao tu. Bali wawe watumishi wa Mwenyezi Mungu katika kuyagawanya kwa wanaostahiki. Basi ikiwa wanajitumilia wao tu bila ya kuwapa hao wanaostahiki wanachukua mizigo ya dhulma kubwa kabisa.

kumuamini Mola wenu; naye Amekwishachukua ahadi kwenu; ikiwa nyinyi ni wenye kuamini (basi aminini).

9. Yeye ndiye Anayeteremsha Aya zilizo wazi juu ya mja Wake ili kukutoeni katika giza mwende kwenye nuru; na bila shaka Mwenyezi Mungu ni Mpole kwenu, Mwenye rehema.

10. Na mumekuwaje, (kwa nini) hamtowi katika njia ya Mwenyezi Mungu — na urithi wa mbingu na ardhi ni wa Mwenyezi Mungu? Hawawi sawa miongoni mwenu wale waliotowa kabla ya kushinda (kwa kutekwa Makka) na wakaendelea kupigana. (Masahaba) hao wana daraja kubwa zaidi kuliko wale ambao wametoa baadaye na wkapigana. Na Mwenyezi Mungu Amewaahidia wema wote hao. Na Mwenyezi Mungu Anazo habari za (yote) mnayoyatenda.

11. Ni nani atakayempa Mwenyezi Mungu karadha nzuri (kwa kutoa Zaka na sadaka na kheri nyinginezo) ili Amzidishie mara nyingi (hapa duniani) na apate malipo mazuri (Akhera).

12. Siku utakapowaona Waislamu wanaume na Waislamu wanawake, nuru zao zinakwenda mbele yao na kuliani kwao; (wanaambiwa:) “Furaha yenu leo; (mnapewa) mabustani yapitayo mito mbele yake kukaa humo daima; huku ndiko kufauli kukubwa, (kufuzu kukubwa).

13. Siku Watakaposema wanafiki anaume na wanafiki wanawake kuwaambia walioamini: “Tungojeeni ili tupate mwangaza katika nuru yenu.” Waambiwe (kwa stihizai): “Rudini nyuma yenu mkatafute nuru yenu. (Labda mumeisahau).” Utiwe baina yao ukuta wenye mlango; ndani yake mna rehema na nje kwa upande wake wa mbele kuna adhabu.

14. (Wanafiki hawa) Watawaita (hawa Waislamu wawaambie:) Je! Hatukuwa pamoja nanyi? (Waislamu) watawaambia; “Ndiyo, walakini nyinyi mlijitia wenyewe katika ukafiri (baada ya kuwa Waislamu), na mkangojea (mabaya yawafike Waislamu), mkajitia shaka (zisizokuwa na sababu), na matamania ya nafsi (zenu) yakakudanganyeni,

لَتُؤْمِنُوا بِرَبِّكُمْ وَقَدْ أَخَذَ مِيثَاقَكُمْ إِنْ كُنْتُمْ مُؤْمِنِينَ ۝

هُوَ الَّذِي يُنَزِّلُ عَلَى عَبْدٍ آيَاتٍ بَيِّنَاتٍ لِّيُخْرِجَكُمْ مِنَ الظُّلُمَاتِ إِلَى النُّورِ وَإِنَّ اللَّهَ بِكُمْ لَعَزِيزٌ ۝

وَمَا لَكُمْ أَلَّا تُنْفِقُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَلِلَّهِ مِيرَاثُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ لَا يَسْتَوِي مِنْكُمْ مَنْ أَنْفَقَ مِنْ قَبْلِ الْفَتْحِ وَقَتْلَ أَوْلِيكَ أَعْظَمُ دَرَجَةً مِنَ الَّذِينَ أَنْفَقُوا مِنْ بَعْدِ وَقَتْلُوا ۚ وَكُلًّا وَعَدَّ اللَّهُ الْحُسْنَىٰ وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرٌ ۝

مَنْ ذَا الَّذِي يُقْرِضُ اللَّهَ قَرْضًا حَسَنًا فَيُضْعِفُهُ لَهُ ۖ لَهُ أَجْرُكَرِيمٌ ۝

يَوْمَ تُرَى الْمُؤْمِنِينَ وَ الْمُؤْمِنَاتِ يَسْعَى نُورُهُمْ بَيْنَ أَيْدِيهِمْ وَبِأَيْمَانِهِمْ بُشْرُكُمُ الْيَوْمَ جَنَّتْ تَجَرَّتْ مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خُلِدِينَ فِيهَا ذَلِكَ هُوَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ۝

يَوْمَ يَقُولُ الْمُنْفِقُونَ وَالْمُنْفِقَاتُ لِلَّذِينَ آمَنُوا انظُرُونَا نَقْتِسِسْ مِنْ تَوَرَّكُم ۖ قِيلَ ارْجِعُوا وَرَاءَكُمْ فَالْتَمِسُوا نُورًا فَضُرِبَ بَيْنَهُمْ بِسُورٍ لَهُ بَابٌ مَبْطُونٌ فِيهِ الرَّحْمَةُ وَظَاهِرٌ مِنْ قَبْلِهِ الْعَذَابُ ۝

يَنَادُوهُمْ أَلَمْ تَكُنْ مَعَكُمْ ۖ قَالُوا بَلَىٰ وَلَكِنَّكُمْ فَتَنْتُمْ أَنْفُسَكُمْ وَتَرَبَّصْتُمْ وَارْتَبْتُمْ وَغَرَّتْكُمُ

10. Hapa zinatajwa fadhila za Masahaba wote kabisa — khasa wale wa mwanzo kabisa — kama ilivyo katika Aya ya 100 ya Suratut Tawba na Aya ya 18 na 29 za Suratut Fat-h na nyinginezo.

hata amri ya Mwenyezi Mungu ikaja na mdanganyu, (Ibilisi) amekudanganyeni katika (habari za) Mwenyezi Mungu.”

15. “Basi leo hakitapokelewa kwenu kikomboleo wala kwa wale waliokufuru (wengine). Makazi yenu ni Motoni; ndio unaokustahikieni; nao ni marejeo mabaya kabisa.”

16. Je! Wakati haujafika tu kwa wale walioamini kwamba nyoyo zao zinyenyekee kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu na kwa mambo ya haki yaliyoteremka? Wala wasiwe kama wale waliopewa Kitabu zamani, (Mayahudi na Manasara), na muda wao (wa kuondokewa na Mitume) ukawa mrefu; kwa hivi nyoyo zao zikawa ngumu, na wengi wao wakawa maasi.

17. Jueni ya kuwa Mwenyezi Mungu Huihuisha ardhi baada ya mauti yake. Bila shaka Tumekubainishieni alama (za uweza wetu wa kuweza kufufua) ili mpate kufahamu.

18. Kwa hakika wanaume watoao sadaka na wanawake watoao sadaka na wale wanaompa Mwenyezi Mungu karadha nzuri (kwa kuongoza katika hayo masadaka na mazaka), watazidishiwa mardufu (papa hapa ulimwenguni) na wapate malipo mazuri (Akhera).

19. Na wale waliomuamini Mwenyezi Mungu na Mitume yake, hao ndio Masidiki na Mashahidi mbele ya Mola wao; watapata malipo yao na nuru yao. Lakini waliokufuru na kukadhibisha Aya Zetu, hao ndio watu wa Motoni.

20. Jueni ya kwamba maisha ya dunia ni mchezo na upuuzi na pambo na kufaharishana baina yenu (kwa nasaba), na kufaharishana kwa mali na watoto. (Na hali ya kuwa vyote hivi hamdumu navyo. Mfano wake) ni kama mvua ambayo huwafurahisha (wakulima) mazao yake, kisha yanakauka ukayaona yamepiga umanjano (badala ya kupiga uchanikiwiti), kisha yanakuwa mabuwa (hayana chochote). Na Akhera kuna adhabu kali (kwa wabaya); na (pia) msamaha wa Mwenyezi

الْأَمَانِي حَتَّىٰ جَاءَ أَمْرُ اللَّهِ وَخُرِكُمْ بِإِلَهِ
الْفُرُورِ ⑩

فَالْيَوْمَ لَا يُوْخَذُ مِنْكُمْ فِدْيَةٌ وَلَا مِنَ الَّذِينَ
كَفَرُوا مَا لَكُمْ الشَّارِدُ هِيَ مَوْلَكُمْ وَبِئْسَ
الْمَصِيرُ ⑪

أَلَمْ يَأْنِ لِلَّذِينَ آمَنُوا أَنْ تَخْشَعَ قُلُوبُهُمْ
لِذِكْرِ اللَّهِ وَمَا نَزَلَ مِنَ الْحَقِّ وَلَا يَكُونُوا
كَالَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ مِنْ قَبْلُ فَطَالَ عَلَيْهِمُ
الْأَمَدُ فَكَفَسَتْ قُلُوبُهُمْ وَكَثِيرٌ مِنْهُمْ
فَسِقُونَ ⑫

إِعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ يُحْيِي الْأَرْضَ بَعْدَ
مَوْتِهَا قَدْ بَيَّنَّا لَكُمْ الْآيَاتِ لَعَلَّكُمْ
تَعْقِلُونَ ⑬

إِنَّ الْمَصْدِقَيْنِ وَالْمَصْدَقَاتِ وَأَقْرَضُوا اللَّهَ
قَرْضًا حَسَنًا يَضَعُ لَهُمْ وَلَهُمْ أَجْرٌ كَرِيمٌ ⑭

وَالَّذِينَ آمَنُوا بِاللَّهِ وَرُسُلِهِ أُولَٰئِكَ هُمُ
الصِّدِّيقُونَ وَالشَّهَادَةُ عِنْدَ رَبِّهِمْ لَهُمْ أَجْرُهُمْ
وَنُورُهُمْ وَالَّذِينَ كَفَرُوا وَكَذَّبُوا بِآيَاتِنَا
أُولَٰئِكَ أَصْحَابُ الْجَحِيمِ ⑮

إِغْلَبُوا إِنَّمَا الْحَيَاةُ الدُّنْيَا لَعِبٌ وَلَهُمْ
وَزِينَةٌ وَتَفَاخُرٌ بَيْنَكُمْ وَتَكَاثُرٌ فِي
الْأَمْوَالِ وَالْأَوْلَادِ كَمَثَلِ غَيْثٍ أَعْجَبَ الْكُفَّارَ
نَبَاتُهُ ثُمَّ يَهَيِّجُ فَتَرَهُ مُصْفَرًّا ثُمَّ يَكُونُ
حُطَامًا وَفِي الْآخِرَةِ عَذَابٌ شَدِيدٌ وَمَغْفِرَةٌ

19. Masiddiqi na Mashahidi ni katika wenye daraja kubwa kabisa baada ya Mitume kwa mema yao makubwa waliyoyafanya. Na hao Mashahidi ni wale waliopata bahati nzuri ya kufa katika midani za vita vya kupigania Uislamu.

Katika hii Aya waliyoifanya ni ya 20 wametia ukafiri wao wa kuthubutisha Utume baada ya Nabii Muhammad (s.a.w.) Na tumebainisha ukafiri huu mahala pengi. Na mahala pa mwisho tulipotaja kwa urefu ni katika Aya ya 40 ya *Suratul Ahzaab*.

Mungu na radhi (Yake kwa wema). Na hayakuwa maisha ya dunia ila ni starehe idanganyayo; (mara huondoka).

21. Yaendeeni upesi (mambo ya kukupatieni) samahani ya Mola wenu na Pepo ambayo upana wake ni kama upana wa mbingu na ardhi, iliyowekewa wale wanaomuamini Mwenyezi Mungu na Mitume yake. Hiyo ni fadhila ya Mwenyezi Mungu, Humpa Amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye fadhila kuu (kabisa juu ya viumbe vyake).

22. Hautokei msiba katika ardhi wala katika nafsi zenu ila umekwishaandikwa katika Kitabu (cha Mwenyezi Mungu) kabla Hatujauumba. Kwa yakini hilo ni sahali kwa Mwenyezi Mungu.

23. Ili msihuzunike sana juu ya kitu kilichokupoteeni (na kinachokupoteeni), wala msifurahi sana kwa Alichokupeni (na kwa anachokupeni). Na Mwenyezi Mungu Hampendi kila ajivunaye, ajifaharishaye

24. Ambao wanafanya ubakhili (wao wenyewe) na kuwaamuru watu wafanye ubakhili (katika mambo ya kheri). Na ageukaye, Mwenyezi Mungu hana haja naye, kwani Mwenyezi Mungu ni Mkwasu, Mwenye kusifiwa.

25. Kwa hakika Tuliwapeleka Mitume Wetu kwa dalili waziwazi na Tukaviteremsha Vitabu na uadilifu pamoja nao, ili watu wasimamie uadilifu. Na Tumekiteremsha, (tumekiumba) chuma, chenye nguvu nyingi na manufaa kwa watu; na ili Mwenyezi Mungu Ajulishe anayemnusuru na Mitume yake, na hali ya kuwa hawamuoni Mwenyezi Mungu. Kwa yakini Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu Mwenye kushinda.

22-23. Wanakatazwa watu; wasivunjike moyo wanapoharibikiwa, bali waanze tena kwa moyo thabiti. Na wakiharibikiwa tena, nawafanye vivyo hivyo. Mwisho watatengenekewa tu. Na wanakatazwa vile vile wasideke wakajiregeza kupuza wanapokuwa wanatengenekewa. Inataka waendele tu kuwa wamacho kila wakati, wasije wakaharibikiwa wakasalia kulia na kusema:

Pete ile
Kiivaa
Zama sizo

Kwanza yalikuwa yangu
Kadiri ya chanda changu
Wanaivaa wenzangu.

25. Makadiyani Katika Aya hii waliyoifanya ya 26 wamekataa tena itikadi ya kuteremka Nabii Isa mwisho wa ulimwengu. Na hivi ndivyo alivyosema Mtume kama tulivyobainisha mahala pengi. Na ulamaa wote wa Hadithi wakataja katika vitabu vyao: "Mlango wa kutaja kuteremka Nabii Isa mwisho wa ulimwengu." Na sasa naongezea nasema: Hadithi za kusema kuwa Nabii Isa atateremka mwisho wa ulimwengu wamezitaja ulamaa wote wa Hadithi:

(a) Imam Al Bukhary amezitaja mara 6; (b) Imam Muslim amezitaja mara 10; (c) Imam Ahmad bin Hambal amezitaja mara 13; (d) Imam Abu Daud amezitaja mara 3; (e) Imam Attirmidhy amezitaja mara 3; (f) Imam Ibni Majah amezitaja mara 3; (g) Imam Al Hakim amezitaja mara 3; (h) Imam An Nasai ametaja mara 1; (i) Imam Attabarany ametaja mara 1. Na wengineo. Basi hatutaacha itikadi aliyotufundisha Mtume kwa maneno yao.

مِّنَ اللَّهِ وَرِضْوَانٌ مَّا الْحَيَاةُ الدُّنْيَا
إِلَّا مَتَاعُ الْغُرُورِ ①

سَابِقُونَ إِلَى مَغْفِرَةٍ مِّن رَّبِّكُمْ وَجَنَّةٍ
عَرْضُهَا كَعَرْضِ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ ۚ أُعِدَّتْ
لِلَّذِينَ آمَنُوا بِاللهِ وَرُسُلِهِ ۚ ذَلِكَ فَضْلُ
اللهِ يُؤْتِيهِ مَن يَشَاءُ ۚ وَاللهُ ذُو الْفَضْلِ
الْعَظِيمِ ②

مَا أَصَابَ مَن مُّصِيبَةٍ فِي الْأَرْضِ وَلَا فِي
أَنفُسِكُمْ إِلَّا فِي كِتَابٍ مِّن قَبْلِ أَن
تَبْرَأَهَا ۚ إِنَّ ذَٰلِكَ عَلَى اللهِ يَسِيرٌ ③
لِّكَيْلَا تَأْسَوْا عَلَىٰ مَا فَاتَكُمْ وَلَا تَفْرَحُوا
بِمَا آتَاكُمْ ۚ وَاللهُ لَا يُحِبُّ كُلَّ مُخْتَالٍ
فَخُورٍ ④

الَّذِينَ يَبْخُلُونَ وَيَأْمُرُونَ النَّاسَ بِالْبُخْلِ ۚ
وَمَن يَسْتَوِلْ فَإِنَّ اللهَ هُوَ الْغَنِيُّ الْحَمِيدُ ⑤

لَقَدْ أَرْسَلْنَا رُسُلَنَا بِالْبَيِّنَاتِ وَأَنزَلْنَا
مَعَهُمُ الْكِتَابَ وَالْمِيزَانَ لِيَقُومَ النَّاسُ
بِالْقِسْطِ ۚ وَأَنزَلْنَا الْحَدِيدَ فِيهِ بَأْسٌ
شَدِيدٌ وَمَنَافِعُ لِلنَّاسِ وَلِيَعْلَمَ اللهُ مَن
يَبْصُرُهُ وَرُسُلَهُ بِالْغَيْبِ ۚ إِنَّ اللهَ
قَوِيٌّ عَزِيزٌ ⑥

26. Na bila shaka Tulimpeleka Nuhu na Ibrahimu, na Tukauweka katika kizazi chao Unabii na Kitabu, lakini wengine katika wao walikuwa waongofu na wengi katika wao walikuwa maasi.

27. Kisha Tukawafuatisha nyuma yao Mitume wetu (wengine) na Tukamfuatisha Isa bin Mariamu, na Tukampa Injili, na Tukauweka upole na rehema katika nyoyo za wale waliomfuata. Na uruhubani (Wanaume kutooa na Wanawake kutoolewa) wameubuni (wenyewe), Sisi Hatukuwaandikia hayo. (Wenyewe walifanya haya) ili kuitaka radhi ya Mwenyezi Mungu. Lakini hawakuufuata (huo Uruhubani wao) kama inavyotakiwa kuufuata. Basi Tukawapa wale walioamini miongoni mwao ujira wao, na wengi wao ni maasi.

28. Enyi mlioamini! Mcheni Mwenyezi Mungu na muaminini Mtume Wake; Atakupeni sehemu mbili (na zaidi) katika rehema Zake, na Atakufanyieni nuru ya kwenda nayo (Akhera), na Atakughufirieni; na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu

29. Ili watu waliopewa Vitabu wajue ya kwamba wao hawana uweza wowote juu ya fadhila za Mwenyezi Mungu; na kuwa fadhila zote zimo mikononi mwa Mwenyezi Mungu, Humpa Amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye fadhila kuu.

وَلَقَدْ أَرْسَلْنَا نُوحًا وَإِبْرَاهِيمَ وَجَعَلْنَا فِي ذُرِّيَّتِهِمَا النُّبُوَّةَ وَالْكِتَابَ فَمِنْهُمْ مُهْتَدٍ وَكَثِيرٌ مِنْهُمْ فَسِقُونَ ﴿٢٦﴾

ثُمَّ قَفَّيْنَا عَلَىٰ آثَارِهِم بِرُسُلِنَا وَقَفَّيْنَا بِعِيسَى ابْنِ مَرْيَمَ وَآتَيْنَاهُ الْإِنجِيلَ وَجَعَلْنَا فِي قُلُوبِ الَّذِينَ اتَّبَعُوهُ رَأْفَةً وَرَحْمَةً وَرَهَابَ لِلَّذِينَ ابْتَدَعُوا مَا كُنْتُمْ عَلَيْكُمْ إِلَّا ابْتِغَاءَ رِضْوَانِ اللَّهِ فَمَا رَعَوْهَا حَقَّ رِعَايَتِهَا فَآتَيْنَا الَّذِينَ آمَنُوا مِنْهُمْ أَجْرَهُمْ وَكَثِيرٌ مِنْهُمْ فَسِقُونَ ﴿٢٧﴾

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَآمِنُوا بِرُسُلِهِ يُؤْتِكُمْ كِفْلَيْنِ مِنَ الرَّحْمَةِ وَيَجْعَلَ لَكُمْ نُورًا تَمْشُونَ بِهِ وَيَغْفِرَ لَكُمْ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٢٨﴾

إِنَّمَا يَعْلَمُ أَهْلَ الْكِتَابِ إِلَّا يَقْدِرُونَ عَلَىٰ شَيْءٍ مِّن فَضْلِ اللَّهِ وَأَنَّ الْفَضْلَ بِيَدِ اللَّهِ يُؤْتِيهِ مَن يَشَاءُ وَاللَّهُ ذُو الْفَضْلِ الْعَظِيمِ ﴿٢٩﴾

27. Mambo mazito yaliyopindukia mipaka — seuze yasiyomkinika — Mwenyezi Mungu hawaamrishii waja wake, kama huko kucha Mungu kwa kutooa au kutoolewa. Basi huu ni uzushi tu waliouzua Manasara pamoja na chungu ya mengine waliyoyazua. Na haya ya kutooana yaliwashinda kuyatekeleza; na mpaka leo yanawashinda. Wanadanganya tu juu juu.

Ujane una simanzi
Ujane una majonzo
Wala mtu hauwezi
Autakaye ujane

Na mashaka na mavune
Na mawazo nane nane
Bure asijidanganye
Asishe kutuhumiwa.